Nipashe
Jumamosi Novemba 16, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580077
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Ofisa Mtendaji atiwa mbaroni kwa madai kifo cha mahabusi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wabunge wanne wa Chadema matatani

**MAHAKAMA** yaamuru wakamatwe, kisa kuruka dhamana, wadhamini wao kikaangoni...*Endelea ukurasa wa 2*



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na viongozi wengine wa chama hicho, wakijadiliana jambo nje ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi inayowakabili kuahirishwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## RAIS TEC ATOA NENO UCHAGUZI WA MITAA

UKURASA 3


Scan Hapa
Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

## Mkapa aeleza sababu kumteua Sumaye kuwa Waziri Mkuu

UKURASA 2

**MICHEZO** KILIMANJARO QUEENS MORALI JUU IKIIVAA SUDAN CHAMAZI UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Hospitali mikoa kusafisha figo

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeahidi kuanza kutoa huduma za usafishaji wa figo katika hospitali za rufani za mikoa ili wananchi wapate huduma kwa muda stahiki katika maeneo yao.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugulile, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Maghembe, wakati akifungua mkutano wa sita wa Chama cha Wataalamu wa Figo jijini.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha hospitali zote za rufaa za mikoa zinaanza kutoa huduma za usafishaji wa figo. Hii ni hatua kubwa sana kwa taifa, lakini pia serikali imeacha milango wazi kwa hospitali na mashirika binafsi kutoa huduma hizo za usafishaji wa figo nchini," alisema.

Alisema hospitali za rufaa ikiwamo Ndada mkoani Mtwara, pia zinatarajia kuanza kutoa huduma hiyo sambamba na hospitali ambazo zinatoa huduma hiyo za Bugando (Mwanza) na Kanda ya Mbeya.

"Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, imehakikisha tunapunguza rufaa za kwenda nje ya nchi na tayari wagonjwa 51 wameshapandikizwa figo nchini," alisema.

Aliwataka wataalamu hao kushawishi vyuo vya utoaji huduma za afya nchini kutoa mafunzo kwa wauguzi ya kusaidiana kutibu wagonjwa wa figo ili kurahisisha huduma za matibabu.

Daktari Bungwa wa Figo, Dk. Onesmo Kisanga, alisema nchini kuna wataalamu 18 wa figo na chama hicho kimeanzishwa kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii namna ya kuepuka magonjwa hayo.

Alisema tathimini iliyofanyika Kaskazini mwa Tanzania miaka mitatu iliyopita, inayonyesha asilimia saba ya Watanzania wana matatizo sugu ya magonjwa.

Dk. Kisanga alitumia fursa hiyo kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kupima ugonjwa wa figo kwa kuwa gharama zake ni Sh. 5,000.

Alitaja sababu za maambukizo ya ugonjwa huo kuwa ni kuzaliwa na tatizo, matumizi ya dawa za kuzuia maumivu, matumizi ya dawa za kienyeji na uzito mkubwa wa mwili.

# Wabunge wanne Chadema matatani

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imetoa amri ya kukamatwa wabunge wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kufikishwa mahakamani kwa kukiuka masharti ya dhamana akiwamo Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Bunda Mjini , Ester Bulaya, John Heche wa Tarime Vijijini na Peter Msigwa wa Iringa Mjini ambao wote na wenzao watano wanakabiliwa na mashtaka ya 13 ya uchochezi.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya washtakiwa hao kushindwa kufika mahakamani wakati kesi yao ilipopangwa kuendelea kusikilizwa.

Vigogo hao wa Chadema wameshindwa kufika mahakamani bila kutoa au kuwapo taarifa kutoka kwao na wadhamini wao.

Awali kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa ushahidi wa mshtakiwa wa kwanza, Mwenyekiti wa Taifa Chadema, Freeman Mbowe, ikiwamo kuhojiwa na mawakili wa Jamhuri. Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alidai kuwa washtakiwa wanne hawako mahakamani na kwamba Jamhuri hawana taarifa, hivyo kuomba mahakama kutoa hati ya kukamatwa kwa kukiuka masharti ya dhamana.

Hakimu Simba alisema jana kesi hiyo ilipangwa kuendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi kuanzia saa 3:00 asubuhi.

Alisema mahakama yake inatoa hati ya kukamatwa washtakiwa hao wanne kwa kukiuka masharti ya dhamana na kutoa hati ya wito kwa wadhamini wao kwenda kujieleza kwanini hawakuwapeleka washtakiwa kusikiliza kesi yao kama masharti ya dhamana yanavyowaelekeza.

Wakili wa utetezi, Faraji Mangula, alidai ameshika mikoba ya mawakili wa utetezi, Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala na Jeremiah Mtobesya kwamba ana taarifa za Bulaya.

Hata hivyo, Hakimu alimwelekeza Wakili Mangula kwamba mwenye jukumu la kutoa taarifa za mshtakiwa ni mdhamini na si kazi ya wakili.

Wakili Nchimbi aliiomba Mahakama itoe hati ya kuwakamata washtakiwa hao na wito kwa wadhamini wao ili wajieleze kwa nini hawakuwapeleka washtakiwa mahakamani kama masharti ya dhamana yanavyotaka.

Mahakama hiyo iliridhia imetoa amri ya kukamatwa washtakiwa na wito kwa wadhamini, Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi Novemba 19, 20 mpaka 21, mwaka huu.

Washtakiwa waliofika mahakamani hapo jana ni Mbowe, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu Bara na Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Dk Vincent Mashinji na Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko.

Katika Kesi hiyo Mbowe na wenzake wanaokabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia na kuhamasisha hisia za chuki kwa Watanzania dhidi ya Serikali.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake Tanzania (TWPG), Margaret Sitta (kulia), akizungumza na baadhi ya wajumbe wa umoja huo na Watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakati walipotembelea na kukagua kiwanja chao watakachojenga shule ya wasichana, kilichopo katika Mji wa Kiserikali Mtumba, jijini humo jana. **PICHA: BUNGE**

# Mkapa aeleza sababu kumteua Sumaye

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS mstaafu Benjamin Mkapa ameeleza namna alivyopata taabu kuunda baraza la mawaziri na kuwashangaza wengi alipomteua Fredrick Sumaye kuwa Waziri Mkuu wake.

Sumaye alikuwa Waziri Mkuu wa Mkapa kwa kipindi chote cha miaka 10 kuanzia mwaka 1995 hadi 2005 na kuwa wa kwanza kutumikia nafasi hiyo kwa miaka yote hiyo mfululizo.

Katika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudi Langu), Mkapa anasema kuwa kabla ya kuteua baraza lake hilo, alikwenda kwa mwasisi wa taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na kumuuliza nani wanafaa na nani hawafai kuwamo kwenye baraza lake.

Anasema Mwalimu Nyerere alikataa kushiriki katika uteuzi wa baraza hilo akisema kuwa hilo ni baraza la Mkapa na hawezi kumchagulia watu wa kwenda kufanya naye kazi, hivyo alipaswa kuliunda mwenyewe.

Mkapa anasema kitu pekee ambacho Nyerere alimtaka akizingatie wakati wa uteuzi ni kuteua kwa kuzingatia usawa wa makabila na madhehebu ya dini nchini.

"Ushauri pekee alionipa Mwalimu Nyerere ni kwamba Tanzania ina makabila mengi na watu wa dini tofauti, hivyo aliniambia kuwa lazima nichague kwa kuzingatia uwiano huo," anasema.

Mkapa anaeleza kuwa majibu hayo yalidhihirisha kwamba Mwalimu Nyerere hakupenda kuwaingilia marais, ingawa watu wengi walikuwa na mtazamo kuwa alikuwa akiwaendesha yeye na aliyemtangulia, Alhaji Hassan Mwinyi.

"Kinachofahamika ni kwamba, yeye ni Baba wa Taifa na aliongoza nchi hii kwa miaka 20. Ingawa alikuwa akipenda sana kufuatilia masuala ya maendeleo, lakini hakutuingilia kama watu walivyokuwa wanafikiri," anasema.

Katika kitabu chake hicho, Mkapa anasema anakumbuka sehemu pekee ambayo Mwalimu Nyerere alimshauri ni wakati wa alipotaka kumteua Gavana wa Benki Kuu, uteuzi ambao anakiri ulichukua muda mrefu kuamua nani wa kushika wadhifa huo.

Anasema Mwalimu Nyerere alimpigia simu na kumuuliza ni nani anayetaka kumteua kuwa Gavana wa Benki Kuu na alipomweleza kuwa ni Daudi Balali,

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakikwepa mti uliokatika na kuziba nusu ya barabara ya Umoja wa Mataifa, eneo la jirani na Shule ya Sekondari ya Tambaza, Upanga Magharibi, jijini humo jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Ofisa Mtendaji mbaroni madai kifo cha mahabusi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linamshikilia Ofisa Mtendaji wa Kata ya Magagula wilayani Songea, Rajabu Tamimu (29), kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mahabusi Ferdinand Haule (41).

Inadaiwa kuwa Haule, mkazi wa Kijiji cha Magagula, alifia kwenye chumba cha mahabusi cha ofisi ya Ofisa Mtendaji huyo.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alidai lilitokea Novemba 13, mwaka huu majira ya saa sita mchana kwenye ofisi hiyo.

Maigwa alisema siku hiyo ya tukio, Haule alifariki dunia akiwa kwenye chumba cha mahabusu alikokuwa amewekwa akikabiliwa na tuhuma za kutumia lugha ya matusi dhidi ya Ofisa Mtendaji wa Kata huyo alipokuwa anafuatilia fedha zake.

Alisema Haule na wenzake walikuwa wamefanya kazi ya kuchimba mchanga kwenye Shirika la Masista wa Kanisa Katoliki lililoko Chipole na malipo yao yalikabidhiwa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata huyo.

Kamanda Maigwa alidai kuwa baada ya kufika kwenye ofisi hiyo, Haule aliyekuwa ameongozana na Beatus Komba, alitumia lugha ya matusi dhidi ya Tamimu, ambaye alilazimika kumkamata na kumweka mahabusu.

Alisema baada ya kuwekwa mahabusu, Haule alipandisha hasira na kuanza kujipigiza kwenye ukuta, kitendo kilichosababisha apoteze fahamu na baadaye alifariki dunia.

Kamanda Maigwa alidai mtuhumiwa Tamimu anashikiliwa na Jeshi la Polisi na upelelezi wa tukio hilo unaendelea.

Hata hivyo, alidai uchunguzi wa awali wa kitabibu uliofanywa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, umebaini kifo cha Haule kimesababishwa na maradhi ya shinikizo la damu.

## Rais TEC atoa neno uchaguzi wa mitaa

**Na Marco Maduhu, SHIN**YANGA

RAIS wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga, ameshauri serikali kukaa meza moja na vyama vya siasa ili kushughulikia dosari zilizoukumba uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Amesema si vyema baadhi ya vyama vya siasa kususia uchaguzi huo na anaona kuna haja kutafuta suluhu ya migogoro iliyojitokeza ili ufanyike kwa amani na utulivu.

Nyaisonga aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Jubilei ya Miaka 25 ya Askofu wa Jimbo la Shinyanga, Liberatus Sangu.

Alisema viongozi wa dini hawataki kuona uvunjifu wa amani unatokea katika uchaguzi huo na wanaona kuna haja serikali na viongozi wa vyama vya siasa kurekebisha dosari zilizojitokeza ili kutoathiri uchaguzi huo.

"Naomba sana dosari hizi ambazo zimejitokeza, zishughulikiwe haraka ili kutoathiri uchaguzi huu wa serikali za mitaa.

"Viongozi wakae pamoja na wanasiasa na kulimaliza suala hili, kususia uchaguzi siyo njia sahihi ya kutatua matatizo, sisi tunataka uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu.

"Nawaomba pia Watanzania siku hiyo ya uchaguzi ambao utafanyika tarehe 24 mwezi huu, mjitokeze kwa wingi kwenye kupiga kura ili mkachague viongozi makini, waadilifu na watakaopigania maslahi yenu," alisema.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo akimwakilisha Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliwaomba viongozi wa dini kuombea amani taifa hasa kwenye kipindi hiki cha uchaguzi ambacho kina viashiria vingi vya uvunjifu wa amani.

Katika maadhimisho hayo, Askofu Sangu akitoa shukrani kwa viongozi wa serikali waliohudhuria huku akitoa pongezi kwa Rais John Magufuli kwa utendaji wake wa kazi.

Alisema kuwa kama kuna mtu anampinga kiongozi huyo wa nchi, atakuwa na tatizo kwenye afya ya akili.

Mbali na Waziri Mwakyembe, viongozi wengine waliohudhuria maadhimisho hayo ni pamoja na aliyekuwa Spika wa Bunge, Anne Makinda, wakuu wa wilaya na wabunge.

## Neema ajira mpya 45,000 serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,800 mwaka huu wa fedha, 9,400 kati yao ni wa kada ya afya.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Silafu Jumbe Maufi (CCM).

Mbunge huyo alisema asilimia 18 ya watumishi wa sekta ya afya wanaoajiriwa ni ndogo na haiendani na kasi ya ujenzi wa vituo vya afya nchini.

"Serikali ina mkakati gani kuhusu rasilimali watu inayohitajika kwenye sekta hii?" mbunge huyo alihoji. Akijibu swali hilo, Mwanjelwa alisema kuajiri watumishi kunategemea hali ya upatikanaji wa fedha.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alisema jitihada za serikali za kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wakati zinaonekana kwa kuwa kila mwaka huongeza bajeti ya Wizara ya Afya kwa ajili ya dawa, vifaa tiba, vitendea kazi na majengo.

Hata hivyo, mbunge huyo akahoji mpango wa serikali kuajiri watumishi kwa kuwa majengo ya kutolea huduma yapo na yanaongezeka.

Akijibu swali hilo, Mwanjelwa alisema vibali vya ajira 29,293 kati ya vibali 156,223, sawa na asilimia 18.75 vimetolewa kwa kada ya afya kuanzia mwaka 2015/16 hadi mwaka 2018/19.

Alibainisha kuwa mwaka 2017/18, serikali ilitoa vibali vya kuajiri watumishi 8,000 wa kada za afya na kwamba utekelezaji wake haukuwa kama ulivyotarajiwa kutokana na kujitokeza kwa wataalamu wachache wa kada za afya. Mwanjelwa alisema serikali imeendelea kutoa vibali vya ajira na kufanya msawazisho wa watumishi wa kada za afya kutoka maeneo yenye watumishi kwenda kwenye maeneo yenye uhaba wa watumishi kulingana na bajeti iliyopo.

Alisema utekelezaji wake haukuwa kama ulivyotarajiwa kutokana na kujitokeza kwa wataalamu wachache wa kada za afya.

Swali hilo pia lilimwinua kitini Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyesema wadau wa sekta ya afya walikutana kuzungumzia rasilimali watu katika sekta hiyo.

"Kikao hicho kitawezesha kuja na mikakati madhubuti ya kuongeza rasilimali watu katika sekta ya afya nje ya bajeti ya serikali kwa sababu wadau wapo tayari kutoa fedha ili kuajiri watumishi katika vituo vilivyoboreshwa," alisema.


TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na dalali TAVIR AUCTION MART kwa niaba ya TUJIJENGE TANZANIA LTD

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| Irene Matiku Nyamtonga | Kiwanja | Chalinze | 19/11/2019 |
| Julius Richard Mbaga | Kiwanja | Vikuge- Kongowe Kibaha | 22/11/2019 |
| Ramadhan Mtumwa Seleman | Kiwanja/ Nyumba | Machinjioni- Mnarani Kibaha | 30/11/2019 |
| Ramiya Yahaya Mtumwa | Nyumba | Machinjioni-Karibu na NIDA Kibaha | 30/11/2019 |
| Steven Buchard Lusangano | Kiwanja | Lubakaya -Chanika | 03/12/2019 |
| Angel Mgwabi Michael | Kiwanja | Kibondeni- MKUZA Kibaha | 06/12/2019 |

MASHARTI YA MNADA

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki na Eviction zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

Kwa maelezo zaidi wasiliana na;- TUJIJENGE TANZANIA LTD
TAVIR A/Mart: 0717495311; MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).

215520802

# Wanafunzi milioni 3 wanufaika elimu bure

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwa mpango wa elimu bila malipo, wanafunzi milioni tatu wa shule za msingi na sekondari wamesajiliwa.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Suzan Lyimo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema walimu wa shule za msingi wanafundishwa mitaala sawa na walimu awali.

"Wakati shule za awali ni za msingi sana na ndipo mtoto anapata elimu ya muhimu sana hivyo wanapswa kufundishwa namna ya kulea watoto. Je, serikali haioni umuhimu wa kuwapa kipaumbele walimu hao wa shule za awali," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema katika kipindi cha miaka minne serikali imefanikiwa kuongeza upatikanaji wa elimu.

"Mfano kwa shule za msingi kutoka wanafunzi milioni 8.2 kwa mwaka 2015 hadi milioni 10.6 kwa mwaka 2019, hivyo ndani ya miaka minne tumeongeza wanafunzi Milioni 2.4 kwa shule za msingi miaka hiyo,"alisema.

Kwa upande wa shule za sekondari, Ole Nasha alisema wanafunzi wameongezeka milioni 1.7 kwa mwaka 2015 hadi wanafunzi milioni 3.3 mwaka mwaka huu.

Alisema ndani ya miaka minne kuna ongezeko la wanafunzi wapya zaidi ya 600,000 na ni matunda ya elimu bila malipo.

Kadhalika, alisema serikali imeanza kuifanyia mapitio Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ambapo katika mchakato huo wadau mbalimbali wakiwamo wabunge watapata fursa ya kutoa maoni yao.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema mfumo wa elimu umekuwa ukilalamikiwa na kukosolewa sana.

"Serikali imefanya utafiti wowote kuona kama lawama hizi zina mashiko au la,"alihoji.

Akijibu swali hilo, alifafanua kuwa serikali imekuwa ikipokea maoni mbalimbali ya wadau kuhusu mfumo wa elimu nchini na kuyafanyia kazi.

"Kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu imekuwa ikifanya ufuatiliaji na kupokea mrejesho juu ya mfumo wa elimu nchini,"alisema

Alifafanua kuwa kufuatia mrejesho huo hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kwa lengo la kuboresha elimu.

"Ili kuhakikisha kuwa mfumo wa elimu unaendelea kuwa bora zaidi na wenye ushindani Kikanda na Kimataifa, Serikali imeanza kuifanyia mapitio Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ambapo katika mchakato huo wadau mbalimbali wakiwamo wabunge watapata fursa ya kutoa maoni yao,"alisema.

# Kabudi: Hakuna mstaafu EAC anayedai

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema hakuna aliyekuwa mfanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) iliyovunjika mwaka 1977, anyeidai serikali.

Amesema waliokuwa wafanyakazi wa jumuiya hiyo wapatao 31,831 walilipwa stahiki zao zote zipatazo Sh. bilioni 117.

Aliyasema hayo jana wakati akisoma Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kueleza kuwa serikali haidaiwi hata senti moja kutoka kwa waliokuwa wafanyakazi wa jumuiya hiyo.

Prof. Kabudi alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Salome Makamba, kueleza kuwa kabla ya kuridhia itifati hiyo ni vyema serikali ikawalipa wastaafu wa jumuiya hiyo.

Makamba alisema ni vyema serikali ikalipa mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977

"Ni jambo jema kuridhia itifaki hii inayoonesha kuwajali watumishi wa Jumuiya kwa kuwapa kinga na maslahi mazuri ya kidiplomasia. Hata hivyo, litakuwa jambo la heri zaidi kama serikali itawakumbuka wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 (wanaotoka Tanzania) ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakidai mafao yao bila mafanikio," alisema Makamba.

Alisema wastaafu hao kupuuzwa kwa madai hayo kwa muda wote huo, kunamaanisha kuwa hawakuwa na haki au maslahi ya kidiplomasia kama watumishi wa sasa.

"Tunaitaka serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki kupeleka hoja katika Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki ya kuzitaka nchi wanachama wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwalipa mafao wastaafu wote wa iliyokuwa jumuiya hiyo ili kuondoa dhana iliyojengeka kwamba serikali za nchi zao zimewadhulumu haki yao," alisema Makamba.

Akijibu hoja hiyo, Prof. Kabudi alisema fedha za waliokuwa wafanyakazi wa EAC zilitunzwa nchini Uingereza na zilitumwa katika kila nchi baada ya kuvunjika.

"Hapa Tanzania tulikuwa na wafanyakazi 31,831 na waliingia makubaliano na serikali walipwe Sh. bilioni 117, na wafanyakazi hao walilipwa wote. Na walipewa miezi sita kwa yule ambaye hakuwa ameridhika apeleke malalamiko na hakuna aliyepeleka," alisema Prof. Kabudi.

Alisema baada ya kipindi cha miezi sita kupita walijitokeza wafanyakazi 5,598 wakidai Sh. trilioni 2.15, wakaenda mahakama kuu kufungua kesi lakini walishindwa.

Kabudi alisema wakaenda tena kufungua kesi katika mahakama ya rufaa lakini walishindwa, wakaenda kufungua kesi katika Mahakama ya usuluhisi ya Afrika Mashariki lakini napo walishindwa.

"Na kwa kuwa wameshindwa katika mahakama zote, serikali haiwezi kutoa hisani zaidi ya hiyo, kwa hiyo serikali haidaiwi hata senti tano, Kwa hiyo tuweke rekodi sawa kwamba hakuna mfanyakazi yoyote aliyekuwa EAC anayeidai serikali" alisema Prof. Kabudi.

Prof. Kabudi alisema orodha ya wafanyakazi wote waliolipwa ipo, baadhi yao wako hai na wengine wameshafariki dunia.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Serengeti Breweries Ltd, Mark Ocitti (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Mratibu wa vipindi wa East Africa Television (EATV), Sophia Proches, jijini Dar es Salaam juzi, baada ya mahojiano kupitia kampeni ya Kibiashara Zaidi. **PICHA: EATV**

# Amchoma kisu kisa kumwagiwa maji machafu 'birthday'

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MWANAFUNZI wa mwaka wa tatu katika Chuo cha Ufundi Trade Peramiho wilayani Songea, Grayson Maselin (23), amejeruhiwa na mwanafunzi mwenzake Mosses Ngole (23), kwa kuchomwa kisu shingoni baada ya kummwagia maji machafu siku ya kumbukizi ya kuzaliwa kwake (birthday).

Ngole, mwanafunzi wa mwaka wa nne katika chuo hicho, anadaiwa kumchoma kisu shingoni mwanafunzi mwenzake huyo na kumsababishia jeraha na kuvuja damu nyingi kwenye sherehe hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alidai tukio hilo lilitokea Jumatano majira ya saa saba mchana katika chuo hicho.

Alidai kuwa, siku ya tukio, Ngole alikuwa analazimishwa kumwagiwa maji na kupakwa matope na wanafunzi wenzake ndipo alipopandisha hasira na kufikia uamuzi wa kumchoma kisu mwanafunzi mwenzake huyo.

Kamanda Maigwa alidai mtuhumiwa anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumjeruhi mwanafunzi mwenzake, ambaye kwa sasa amelazwa Hospitali ya Kanisa Peramiho.

# Wizara 'yalia' radi kuharibu transfoma

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WIZARA ya Nishati imesema baadhi ya maeneo transfoma zilizofungwa zinaharibika kutokana na uwapo wa radi.

Imeyataja maeneo yenye kikwazo hicho kuwa ni mikoa ya Kagera, Katavi na Njombe.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema hayo jana bungeni mjini hapa jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Maswa Magharibi, Mashimba Ndaki (CCM).

Mbunge huyo alisema kumekuwa na tatizo la transfoma zinazowekwa na makandarasi wa umeme wa REA kulipuka na kuharibika ndani ya muda mfupi tangu kufungwa kwake.

Ndaki alitaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kutatua tatizo hilo.

Akijibu swali hilo, Mgalu alisema uchunguzi uliofanyika, umeonyesha baadhi ya vifaa vya kulinda transfoma kuathirika na radi, hivyo hushindwa kufanya kazi vizuri na kusababisha transfoma kuharibika zinapopigwa na radi.

Alisema matukio ya wizi wa baadhi ya vifaa na waya za shaba zinazotumika katika mfumo wa ulinzi wa transfoma, pia yamesababisha transfoma kuungua.

Alisema serikali kupitia Tanesco na REA imekuwa ikibaini baadhi ya transfoma kuharibika muda mfupi baada ya kufungwa katika baadhi ya maeneo ya miradi ya umeme vijijini inayofadhiliwa na Mfuko wa Nishati Vijijini (REF).

Vilevile, alisema baadhi ya transfoma, hasa za kutoka nje ya nchi, zimekuwa hazina ubora na serikali imechukua hatua ya kuhakikisha transfoma zote zinazotumika kusambaza umeme, zinatokana na viwanda vya nchini vilivyothibitishwa na Shirika la Viwango (TBS).

"Pia, elimu kwa wananchi imeendelea kutolewa kwa ajili ya ulinzi wa miundombinu ya umeme, zikiwamo transfoma katika maeneo yao ya miradi," alisema.

# MOI yafanya upasuaji ubongo mwenye kifafa

**Na Mary Geofrey**

MADAKTARI bingwa wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Weill Cornell, Marekani, kwa mara ya kwanza nchini wamefanya upasuaji mkubwa wa ubongo kwa mtoto mwenye kifafa.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema hiyo ni hatua kubwa katika matibabu ya ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu nchini. Wagonjwa wenye ugonjwa wa kifafa wanaohitaji upasuaji walikuwa wanapelekwa nje ya nchi.

"Leo (juzi) ni siku ya kongamano lao la kimataifa la madaktari bingwa wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu. Kila mwaka, wenzetu hawa kutoka mataifa ya Amerika na Ulaya wamekuwa wakituletea teknolojia mpya na hii ya upasuaji kwa wagonjwa wenye kifafa ni mojawapo," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo MOI, Dk. Japhet Ngerageza, alisema upasuaji huo umewezekana kutokana na uwapo wa vifaa vya kisasa ambavyo vimenunuliwa na serikali.

"Tunaishukuru sana serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Dk. John Magufuli, kwa uwekezaji mkubwa iliyofanya katika taasisi yetu ya MOI, tunaweza kufanya upasuaji kama huu kutokana na uwapo wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi kama EEG, MRI na darubini ya kisasa ya upasuaji wa ubongo, ambavyo vyote vimenunuliwa na serikali," alisema.

Daktari bingwa wa ubongo kutoka Canada, Dk. Evan Lewis, alisema ni heshima kubwa kuwa sehemu ya kongamano ambalo limetoa huduma upasuaji kwa wagonjwa wa kifafa nchini na kuokoa maisha ya watoto. Alisema upasuaji huo unachukua saa tatu hadi nne.



Dk. Emmanuel Maganga wa Hospitali ya Regency (kulia), akimpa ushauri kuhusu namna ya kuepuka ugonjwa wa kisukari mmoja wa wananchi waliofika kwenye kambi ya kupima ugonjwa bure, iliyoendeshwa na hospitali hiyo, katika eneo la Mlimani City, jijini Dar es Salam juzi.
**PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Daktari aonya ongezeko kisukari

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI wameonya kuwa ugonjwa wa kisukari unaweza kuendelea kuongezeka kama watu hawatabadili mfumo wa maisha na kuachana na ulaji usiozingatia afya.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na daktari wa Regency Medical Center, Dk. Emmanuel Maganga, wakati wa kambi ya kupima ugonjwa huo bure.

Dk. Maganga anayeendesha kambi hiyo, alisema kuna sababu nyingi za kuongezeka kwa maradhi ya kisukari ikiwamo watu kutofanya mazoezi.

Alisema ulaji wa vitu vya mafuta mengi, pombe na sigara, huchangia kwa kiwango kikubwa watu wengi kuishi na maradhi ya kisukari.

"Unakuta mtu anakaa siku nzima ofisini lakini akitoka ndani ya gari hatembei hata nusu kilomita kwa siku na anakula vyakula vya mafuta mengi huyo anakuwa kwenye hatari ya kisukari," alisema Dk. Maganga

Alisema ulaji mkubwa wa vyakula vya kuoka kama chipsi ni moja ya vyanzo vikubwa vya ugonjwa huo na alitahadharisha umma kutopendelea aina hiyo ya vyakula.

Dk. Maganga alisema chanzo kingine cha ugonjwa huo ni kula kwa kuchelewa akitolea mfano mtu anayekula na kwenda moja kwa moja kulala.

Alisema mtu anapopata mlo wa jioni ni vyema akakaa angalau masaa mawili ili chakula kiweze kumeng'enywa na ndipo aende kulala.

Katika kambi hiyo zaidi ya watu 500 walijitokeza kupima bure maradhi ya kisukari katika kambi ya upimaji iliyoendeshwa na hospitali ya Regency ya Upanga jijini Dar es Salaam.

Meneja Utawala wa hospitali hiyo, Ashul Kanabar, aliliambia gazeti hili kuwa wamekuwa wakifanya hivyo kila mwaka kwa ajili ya kuadhimisha siku ya kisukari duniani ambayo iliadhimishwa jana.

Alisema kwenye kambi hiyo wameweka wauguzi na madaktari mbalimbali ambao wamekuwa wakitoa huduma za ushauri nasaha kuhusu namna ya kuishi bila kisukari.

Maganga alisema Novemba 24, mwaka huu, wataendesha kambi kubwa kama hiyo katika ukumbi wa Lohana Mahajan Community katikati ya Jiji ili kuwapima watu maradhi hayo.

Kanabar alisema madaktari hao wamekuwa wakiwapa ushauri hata wale wenye kisukari namna ya kuishi na ugonjwa huo bila kuwaletea madhara.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili dirisha dogo klabu Ligi Kuu uzingatie haya

**UMEBAKI** mwezi mmoja kabla ya dirisha dogo la usajili kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara kufunguliwa rasmi mwezi ujao Desemba 16, ambao utadumu hadi Januari 15, mwakani.

Na wakati huu Ligi Kuu Bara ikiwa mapumzikoni kupisha kalenda ya mechi za kimataifa, tayari klabu mbalimbali zimeanza kuanika mikakati yao ya usajili kuelekea dirisha hilo mwezi ujao.

Hata hivyo, kinachoshangaza ni kukutana na taarifa zinazowanukuu baadhi ya makocha wakipania kufanya mapinduzi makubwa katika vikosi vyao kwa kufyeka idadi kubwa ya wachezaji pindi dirisha hilo litakapofunguliwa.

Kauli hizo zinatokana na baadhi ya timu kufanya mabadiliko katika mabenchi yao ya ufundi kwa ama kubadili benchi zima la ufundi au kocha mkuu kutimuliwa na kubaki na kaimu kocha ama makocha wasaidizi, ambao wanaamini kuunda vikosi vyao kwa kusajili wachezaji wanaowataka. Hata hivyo, wakati huu ambao tumeshuhudia timu nyingi zikipata wakati mgumu katika kuwaunganisha wachezaji waliowasajili kutokana na wengi wao kuwa wapya, hatutarajii tena kuona kukifanyika mabadiliko makubwa ya wachezaji katika klabu hizo wakati wa dirisha dogo la usajili.

Nipashe kama mdau aliyebobea tangu enzi katika soka, linafahamu dirisha dogo ni kwa ajili ya kuziba mapengo machache sana yaliyojitokeza husuan idara ambazo zimekabiliwa na majeruhi wa muda mrefu au mchezaji husika kushindwa kuonyesha uwezo katika mzunguko wa kwanza.

Hivyo, usajili mkubwa unaosemwa kuelekea dirisha dogo ni wazi utazidi kuziathiri timu zitakazofanya hivyo, kwa kulazimika kuhitaji tena muda mrefu ili wachezaji kuweza kuzoeana, jambo ambalo tumeona ni vema kulitahadharisha mapema.

Lakini pia duniani kote, katika kipindi cha dirisha dogo si rahisi kupata wachezaji wa kiwango cha juu kama ilivyo kwa dirisha kubwa, hivyo ni vizuri makocha ama kamati za usajili za klabu husika kuelekeza malengo yao katika kusajili wachezaji kwa ajili ya kuziba nafasi zilizoachwa kutokana na majeruhi ama mchezaji husika kupwaya na si kufanya mapinduzi makubwa kikosini.

Tunataka kuona klabu zetu zikiimarika zaidi si tu kwa kuwa na wachezaji wazuri, bali waliokaa kwa pamoja kwa muda mrefu na kuzoeana na hatimaye kutoa ushindani chanya kwenye michuano hususan ya kimataifa.

Sote tulishuhudia namna ambavyo klabu za Tanzania Bara, Simba, Yanga, Azam, KMC na hata zile za Zanzibar KMKM na Malindi zilivyotolewa mapema kwenye michuano ya kimataifa na kujikuta zikishindwa kutinga hatua ya makundi ambapo utajiri wa fedha huanzia. Kisingizio ama malalamiko kwa klabu hizo kutolewa mapema, kimekuwa ni michuano hiyo msimu huu, eti kuwahi kufanyika kinyume cha ilivyozoeleka misimu iliyopita, jambo ambalo wachezaji wao walikuwa hawajazoeana vizuri.


Hilo tunaweza kukubaliana nalo, lakini pia hatuna budi kujiuliza je, imefanyika mapema kwa klabu za hapa nchini tu ama ni kwa zote zinazoshiriki michuano hiyo ya kimataifa barani Afrika?

Jibu la swali hilo, linaonyesha ni kwa namna gani ilivyo muhimu kwa klabu za soka nchini kujenga utamaduni wa kutopenda kupomoa vikosi vyao kila msimu huku vikisajili zaidi ya wachezaji wapya sita ambao wanapaswa kuingizwa moja kwa moja kikosi cha kwanza.

Kwa kutambua hilo, hatutarajii kuona tena likijitokeza kipindi hiki cha dirisha dogo ambalo ni mahususi kwa kuziba mapengo machache yaliyojitokeza kutokana na kuwapo kwa majeruhi.

Sambamba na hilo, klabu hazina budi kufuata utaratibu uliowekwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kutangaza mapema wachezaji watakaoachwa ili kuwafungulia soko kwingineko badala ya kusubiri hadi zikiwa zimebaki siku mbili ama tatu kabla ya dirisha hilo kufungwa ndipo waanike walioachwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wa kulaumiwa Simba si Aussems peke yake

Na Adam Fungamwango

**SIKU** chache baada ya klabu ya Yanga kumuondosha kocha wake mkuu Mwinyi Zahera, ni kama bundi ametoka maeneo ya Jangwani na kuanza kuambaa kwenye mitaa ya Msimbazi.

Tayari baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba wameanza kumnyooshea kidole cha shahada Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems, si tu kutokana na matokeo hafifu ya siku za karibuni, bali wanaonekana kutoridhishwa hata na aina ya soka linalochezwa na kikosi chao.

Wanachama na mashabiki wa Simba wanaonekana bado kuwa na dukuduku la kutolewa mapema kwenye michuano ya Ligi Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji.

Wanaonekana kama hawakutaka tu kuonyesha hasira zao wakati huo, baada ya kupozwa hasira zote sasa zitaelekezwa kwenye Ligi Kuu na hakuna timu ya kuisimamisha Simba.

Baada ya kuvumilia ilipochapwa na Mwadui bao 1-0, sare ya nyumbani ya bila kufungana dhidi ya Prisons imewafanya kutoa dukuduku lao wakisema kuwa Mbelgiji huyo ameishiwa mbinu, hivyo ni wakati sasa wa kuaondolewa.

Ni kweli kabisa Simba iliondolewa kizembe na UD Songo, kwani ukiangalia mwenendo wa timu hiyo baada ya hapo, ilifungwa mechi zote nne za nyumbani na ugenini.

> **Ni kweli kabisa Simba iliondolewa kizembe na UD Songo, kwani ukiangalia mwenendo wa timu hiyo baada ya hapo, ilifungwa mechi zote nne za nyumbani na ugenini.**

Kwa ninavyoona ni kwamba matatizo ya Simba hayapo kwa kocha Aussems peke yake na hata kama akitimuliwa, matatizo bado yataendelea kuwapo.

Naweza kuainisha matatizo yapo sehemu tatu. Kocha ana sehemu yake ndogo, wachezaji wenyewe na baadhi ya viongozi waliopewa majukumu ya kusajili.

Nikianza na Aussems, nimesikia kuwa hapendi wachezaji wake wakae kambini kwa muda mrefu. Hili linaweza kumgharimu, kwani wachezaji wanaocheza soka Tanzania bado hawajajua kujitunza wenyewe na si kama wa Ulaya.

Kingine kuwachezesha wachezaji wengi wasio na kasi katikati ya uwanja. Sharaf Shiboub, Clatous Chama na Ibrahim Ajibu, wakicheza kwa pamoja, huwezi kuwa na timu inayoshambulia kwa kasi kwa sababu wote asilia yao ni kupaka rangi mpira na hawana kasi.

Ukiacha matatizo ya kocha, baadhi ya wachezaji wa Simba msimu huu kama Jonas Mkude na Chama hawako kwenye viwango vyao vilivyozoeleka, ukichanganya na upangaji wa wachezaji wasio na kasi unaikuta Simba iliyopooza.

Lakini pia wapo wachezaji ambao hawajitumi uwanjani. Unashangaa kuona Simba ina makocha wengi wa viungo na fiziki, lakini wachezaji wengi hawawezi kugombea mpira na wapinzani wakaweza kuuchukua. Wengi wanashindwa nguvu au wanaogopa kuingiza mguu.

Wachezaji wanaoonekana wana uwezo wa kupambana kwa kushindana nguvu ni Meddie Kagere, Paschal Wawa, Gelson Fraga, Hassan Dilunga, na Mzamiru Yassin tu, wengine wote wanaonekana kucheza kigoigoi.

Tatizo la tatu ni viongozi waliofanya usajili msimu huu. Timu kubwa kama ya Simba ina mastraika watatu tu kitu ambacho ni kosa kubwa na ni aibu.

Mfano ingekuwa inaendelea kwenye michuano ya kimataifa ingekuwaje kama ina Kagere tu mbele?

Simba inaonekana kwa kiasi kikubwa inaathirika kwa kukosekana kwa John Bocco. Msimu huu wote tangu uanze imekuwa ikisimamisha straika mmoja tu ambaye ni Kagere, akibanwa inakuwa mtihani kufunga kama winga Miraji Athumani hakusaidia.

Viongozi waliosajili msimu huu, walifanya makosa kwa kusajili straika mmoja tu Mbrazil Wilker Henrique da Silver, ambaye naye inaonekana uwezo wake ni wa kubahatisha.

HABARI KITAIFA

# ‘Hakuna atakayelazimishwa kupiga kura uchaguzi mitaa’

**Na Mary Geofrey**

WAKATI kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zikitarajiwa kuzinduliwa rasmi kesho, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali haimlazimishi wala kumshinikiza mtu yeyote kwenda kupiga kura katika uchaguzi huo.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Tamasha la Sanaa la Mwalimu Nyerere, lililowajumuiya wasanii kwa lengo la kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kupitia sanaa.

Majaliwa alitangaza msimamo huo wakati ambao vyama kadhaa vya upinzani vimejiondoa kushiriki uchaguzi huo kwa madai ya dosari mbalimbali zilizojitokeza katika hatua za awali za kuwapata wagombea.

“Tunataka tuwahakikishie ulinzi na usalama, utulivu na amani vipo mpaka siku ya kupiga kura. Hakuna atakayeshinikizwa, hakuna atakayelazimishwa, kila mmoja aende kwa hiari yake bila vurugu.

“Nenda kituoni, chukua karatasi, weka alama, ingiza kwenye boksi, rudi nyumbani kafanye kazi zako,” alisema Majaliwa. Waziri Mkuu aliwataka Watanzania kutumia haki zao za msingi kujitokeza kushiriki katika uchaguzi huo muhimu wa kuwapata viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji.

“Naomba niwakumbushe lile la tarehe 24, tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni haki yako ya msingi kabisa ya kwenda kumchagua kiongozi wa serikali ya mtaa, kijiji na kitongoji,” alisema.

“Kampeni zinazinduliwa tarehe 17, ni wakati wako wa kwenda kusikiliza anataka kusema nini, lakini mpime kama kweli anaweza kuleta maendeleo. Tunataka tupate viongozi wanaoweza kufanya kazi kwa kuendana na kasi hii ya Rais John Magufuli, ishuke mpaka kule kijijini,” alisema.

Majaliwa pia aliwapongeza wasanii kwa kazi nzuri wanazofanya za kuelimisha jamii kupitia sanaa, ikiwamo kuhamasisha wananchi kujiandikisha kwenye daftari na kwenda kupiga kura siku ya uchaguzi.

Majaliwa pia aliwataka kuunganisha vyama vyote vya wasanii ili kuwa na shirikisho moja ambalo litakuwa na nguvu na kuleta tija kwa taifa. Waziri Mkuu alisema sekta ya sanaa nchini inaendelea kuchangia katika ukuaji wa sekta ya uchumi na mwaka wa fedha wa 2018/19, mchango wake ni asilimia 13.7.

Katika tamasha hilo, zaidi ya Sh. milioni 140 zilipatikana kupitia ahadi zilizotolewa na viongozi mbalimbali akiwamo Rais Magufuli aliyeahidi kutoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuanzisha mfuko wa utamaduni kusaidia wasanii nchini. Mwenyekiti wa Maandalizi ya tamasha hilo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, mbali na kuwashukuru wasanii kwa umoja wao, alimwomba Waziri Mkuu kutilia mkazo fedha za mikopo kwa wajasiriamali zilizoahidiwa kutolewa katika kila halmashauri ili wasanii nao wanufaike. Majaliwa alisisitiza utekelezaji wa agizo hilo lililotolewa na serikali katika kila halmashauri, akieleza kuwa zinapaswa kuwasaidia wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa.



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, akizungumza katika maadhimisho ya miaka 30 tangu kuangushwa kwa ukuta wa Berlin, uliokuwa ukizitenganisha Ujerumani Mashariki na Magharibi, yaliyofanyika jijini Dodoma juzi usiku. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kampeni kuwathamini baba, mama lishe yaja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bingwa Laboratories Limited kupitia bidhaa zake za Emina na kushirikiana na Miriam Lukindo Mauki ambaye ni balozi wa Emina, imezindua rasmi kampeni ya ‘Emina Mbabe wa Usafi’ kwa ajili ya kusaidia baba na mama lishe.

Emina mbabe wa usafi chini ya mpango wa Emina Wapishi Award inalenga kutoa zawadi mbalimbali, mafunzo na semina kwa baba na mama Lishe kwa Tanzania nzima kwa lengo la kuboresha biashara za wajasiriamali hao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Lukindo alisema wanaamini kwa kufanya hivyo Baba na Mama Lishe watathaminiwa zaidi na kuchochea maendeleo yao binafsi, wafanyakazi wao na jamii kwa ujumla.

Alisema lengo kuu ni kutambua mchango mkubwa na nguvu ya Baba na Mama Lishe kijamii, kiuchumi na kiafya.

“Usafi ni afya ndiyo maana tunasema hakuna usafi bila Emina mbabe wa usafi. Kampeni ya Emina mbabe wa usafi itaanzia Mkoa wa Dar Es Salaam na kuendelea Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro kwa awamu ya kwanza kisha itasambaa mikoa mingine ya Tanzania,” alisema Lukindo.

Alisema mpango huu utatekelezwa kwa kuhusisha wadau wenyewe ambao ni Baba na Mama Lishe kwa kushirikiana na viongozi wao kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata na mtaa.

# Bunge lapitisha azimio kumpongeza JPM

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limepitisha azimio la kumpongeza Rais John Magufuli kutokana na utendaji wake mzuri katika miaka minne ya utawala wake.

Akisoma azimio hilo bungeni jana, Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Jasson Rweikiza, alisema katika kipindi hicho cha miezi 48, mambo makubwa yenye tija kwa taifa yamefanyika ambayo yanamgusa kila Mtanzania, hususani wanyonge.

Alisema serikali ya awamu ya tano imesimamia kwa ukamilifu taratibu za makusanyo serikalini ambayo yamesababisha kuongezeka kwa makusanyo ya mwezi kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 hadi Sh. trilioni moja kwa mwezi.

Alisema matumizi ya serikali yasiyo ya lazima pia yamepungua, akitolea mfano safari za nje zisizo na faida wala tija kwa taifa zilizokuwa zinagharimu taifa mabilioni ya shilingi. Alisema Rais Magufuli ameondoa watumishi hewa zaidi ya 10,000 waliokuwa wakilipwa mishahara bure. “Kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne kuanzia Januari, 2016 hadi Oktoba, 2019, Sh. bilioni 987 zimetolewa na serikali na kutumwa moja kwa moja shuleni,” Rweikiza alisema. Alisema mikopo elimu ya juu imeongezeka kutoka Sh. bilioni 341 kwa mwaka hadi Sh. bilioni 450 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, na urejeshwaji wake kutoka Sh. bilioni 28.2 mwaka 2015/2016 hadi Sh. bilioni 183.2 mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 549.65.

Alisema miundombinu imeimarika katika nyanja zote, ukiwamo ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, madaraja na barabara za juu, ujenzi wa reli ya kisasa sambamba na kufufua njia ya reli kutoka Tanga hadi Moshi.

Rweikiza alisema serikali pia imeimarisha viwanja vya ndege na Shirika la Ndege (ATCL) kwa kununua ndege mpya zipatazo nane mpaka sasa. Alisema serikali ya awamu ya tano pia imeimarisha mapambano dhidi ya rushwa kwa kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) pamoja na kuanzisha Mahakama ya Mafisadi.

Alisema pia imeinua sekta ya kilimo kwa kusimamia bei yenye maslahi kwa wakulima wa mazao ya korosho, pamba, kahawa na ufuta.

Alisema serikali pia imeimarisha sekta ya madini kwa kuongeza mapato katika sekta hiyo ikiwamo kutunga sheria zinazosimamia rasilimali na maliasili za nchi kwa manufaa ya nchi, kuanzisha masoko ya madini nchini na ujenzi wa ukuta wa Mirerani.

## Sababu JKT kutochukua wahitimu wote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa sababu tatu Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kutochukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita.

Sababu hizo zilitajwa jana bungeni na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, alipojibu swali la Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia (CCM).

Mbunge huyo alihoji sababu za fursa ya kujiunga na JKT kutolewa kwa vijana wachache na siyo wahitimu wote wa kidato cha sita.

Akijibu swali hilo, Dk. Mwinyi alisema sababu hizo ni ufinyu wa bajeti, uhaba na uchakavu wa miundombinu na mwingiliano wa muda wa kujiunga na JKT na muda wa vijana hao kujiunga na vyuo vikuu.

"Ufinyu wa bajeti unasababisha mafunzo haya kuendeshwa kwa kutumia fedha zinazopatikana toka Hazina na pia kwa kutumia rasilimali zinazopatikana ndani ya Jeshi la Kujenga Taifa," alisema.

Dk. Mwinyi alisema idadi ya vijana wanaojiunga na JKT baada ya kumaliza kidato cha sita inaendana na rasilimali fedha zinazopatikana.

"Kuhusu mwingiliano wa muda wa kujiunga na JKT kwa vijana wa mujibu wa sheria na muda wa kujiunga na vyuo vikuu," alisema.

Alisema mafunzo ya JKT kwa vijana kwa mujibu wa sheria huendeshwa kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Juni hadi Septemba ili kuendana na mihula ya masomo ya elimu ya juu inayoanza Oktoba.

Dk. Mwinyi alisema kama kungekuwa na rasilimali za kutosha na kama kungekuwa na uwezekano wa kuanza mihula ya masomo ya elimu ya juu katika wakati mwingine, ingewezekana kuendesha mafunzo ya vijana hao kwa awamu kadhaa.

"Jeshi la Kujenga Taifa bado linakabaliwa na uhaba na uchakavu wa miundombinu katika kambi zake," alisema.

Alitaja miundombinu hiyo kuwa ni pamoja na majengo na miundombinu ya mazoezi ya kijeshi na kwamba hali hiyo imesababisha JKT kushindwa kuchukua vijana wengi kwa wakati mmoja.

Alisema JKT inaendelea kutumia fedha za maendeleo zinazotolewa na serikali pamoja na vyanzo vya ndani vya mapato katika kuimarisha miundombinu katika kambi zake pamoja na kuboresha miundombinu iliyopo ili kuongeza uwezo wa kuchukua vijana wengi kwa wakati mmoja.

Alisema juhudi hizo zimewezesha kufufuliwa kwa Kambi za Makuyuni, Mpwapwa, Luwa, Milundikwa, Itaka na kujengwa kwa kambi mpya ya Kibiti na kuongeza idadi ya vijana wanaojiunga na JKT.

# Mashauri 11,000 matunzo ya watoto yashughulikiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema mashauri 11,897 yaliyohusu matunzo kwa watoto na wanawake yameshughulikiwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwaka 2018/19.

Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 148 kulinganisha na idadi ya mashauri 11,815 yaliyopokewa katika kipindi cha mwaka 2017/18.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Faida Mohammed Bakar (CCM).

Mbunge huyo alisema wanawake wengi walioachika pamoja na wajane, watoto wao hutelekezwa na kukosa matumizi kutoka kwa baba zao na kusababisha watoto hao kukosa huduma muhimu na wazazi hao wa kike kuteseka.

Kutokana na hali hiyo mbunge huyo alitaka tamko la serikali na hatua zinazochukuliwa dhidi ya kinababa wanaotelekeza watoto wao.

Dk. Ndugulile, akijibu swali hilo, alisema ongezeko hilo ni ishara ya kuongezeka kwa hamasa kwa kinamama wanaotelekezwa kuchukua hatua kwa kufika Ofisi za Ustawi wa Jamii kwa ajili ya utatuzi wa malalamiko yao.

"Ni jukumu la maofisa ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria hii na kanuni zake ipasavyo," alisema.

Alitoa wito kwa wanawake waliotelekezwa na waliotelekezewa watoto, kufika katika Ofisi za Ustawi wa Jamii kwenye halmashauri zao ili hatua stahiki zichukuliwe kwa maslahi ya watoto wao.

"Pia, nitoe wito kwa wazazi na walezi wote nchini kuhakikisha wanatoa huduma bora za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto wao ili wakue vema na kufikia ndoto zao," alisema.

Aliongeza kuwa huduma za matunzo, malezi na ulinzi kwa watoto zinatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 Kifungu cha 7-9, ambavyo vinatoa majukumu kwa wazazi na walezi wote kuhakikisha wanawalea na kuwatunza watoto wao.

Alisema kifungu cha 14 cha sheria hiyo kinatoa adhabu kwa mzazi na mlezi yeyote atakayekiuka, atatozwa faini isiyozidi Sh. milioni tano au kifungo kisichozidi miezi sita gerezani au vyote viwili, faini na kifungo.



Mkurugenzi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, akifungua mkutano wa wadau wa uchaguzi kuhusu nafasi ya mwanamke katika uchaguzi, uliofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mkapa aeleza sababu kumteua Sumaye

**INATOKA UK. 2**

Mwalimu Nyerere hakubisha na huo ukawa mwisho wa mazungumzo yao.

Anasema hatua yake ya kuwatupa nje ya baraza lake mawaziri wakuu wawili wastaafu, uliibua utata, hisia tofauti na iliwashangaza wengi alipoacha majina makubwa kwa wakati huo, lakini iliwafanya wengi watambue kuwa hawakuwa wanamfahamu yeye ni mtu wa aina gani.

"Nilisikia kwamba Mwalimu aliposikia mawaziri wakuu wastaafu wawili hawapo kwenye baraza langu, alisema kuwa 'sikufahamu kwamba mtu huyu ana msimamo namna hii'. Kulikuwa na sababu kwa uamuzi wangu kuhusu watu wenye sifa za kuwamo kwenye baraza langu," Mkapa anasema.

Mkapa anaeleza kuwa lengo lake kuu lilikuwa ni kuweka matarajio ya mabadiliko kwa kuhakikisha baraza lake linatawaliwa na sura nyingi mpya huku akiwatupa nje wakongwe.

Anasema iwapo angewajumuisha Cleopa Msuya na John Malecela ambao walikuwa na nguvu kubwa kwa wakati huo, ingekuwa ngumu kwake kutetea baraza lake kuwa ni lenye kasi ya kuharakisha maendeleo kwa wakati huo.

**SUMAYE WAZIRI MKUU**

Mkapa anasema hatua ya kumteua Sumaye kuwa Waziri Mkuu iliwashangaza wengi kwa kuwa hawakuwa wakimtarajia kuwa na uwezo wa kushika nafasi hiyo.

Anasema faida kubwa aliyokuwa nayo na iliyomwezesha kufanya mambo yake bila kupata msukumo wowote kutoka kwa watu, ni kutokuwa na kundi wakati wa mchakato wa uchaguzi, hivyo haikuwa rahisi kupata shinikizo la kuweka watu kwenye nafasi za uteuzi.

Mkapa anasema wale waliokuwa wakijiweka karibu naye wakitaka upendeleo kutoka kwake, walikuwa wakiwekwa mbali na meneja wake wa kampeni, Ferdinand Ruhinda.

"Alikuwa akiwaambia 'kaa mbali, mwacheni Rais aongoze nchi. Tulikuwa pamoja ili tumwezeshe kushinda na afanye kazi na si kuungana naye baada ya kushinda'. Na uzuri ni kwamba, kampeni za mwaka ule hazikuwa na gharama kubwa, watu walikuwa wakichanga kwa hiyari," anasema Mkapa.

Anasema hakulazimika kuweka watu kwenye nafasi za uteuzi kama zawadi kwa michango mikubwa waliyotoa kwenye chama wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, hivyo alikuwa na uhuru wa kuweka watu kwa kuzingatia umahiri wao na msaada kwa Watanzania.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akizungumza na wakazi wa Kata ya Tlawi, wilayani Mbulu juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Naibu Katibu Mkuu EAC afunguka

**Novatus Makunga,** ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Christophe Bazivamo, amesema elimu ndogo ya uelewa wa taratibu za forodha, imesababisha wajasiriamali wadogo wa mipakani mwa nchi za ukanda huo, kufanyabiashara kwa kutumia njia zisizo rasmi, maarufu kama njia za panya.

Bazivamo alitoa kauli hiyo jana mjini hapa wakati akifungua wiki ya mradi wa kuunganisha wafanyabiashara wadogo mipakani na maendeleo katika Afrika ya Mashariki (IIDEA).

Alisema wafanyabiashara wadogo kutokuzifahamu taratibu mbalimbali zinazosimamia biashara za mipakani, zimewafanya kutumia njia za panya na kushindwa kupata maendeleo. "Mara nyingi kutumia kwao njia za panya kumewagharimu zaidi na hata kuhatarisha maisha yao kwani wanapita maporini na katika njia ndefu sana hadi kufika kule wanakopeleka bidhaa," alisema.

Bazivamo ambaye anahusika na sekta za uzalishaji na jamii katika jumuiya hiyo, alisema hivi sasa kunahitajika mpango endelevu wa kutoa elimu katika jamii, ambao utakuwa msingi wa kuwajengea uwezo wafanyabiashara wadogo.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Biashara la Afrika ya Mashariki (EABC), Peter Mathuki, alisema kasi ya ukuaji wa biashara ya Afrika ya Mashariki ni ndogo ambayo ni asilimia 12.

Alisema katika kipindi cha miaka 20 ya jumuiya hiyo, ilipaswa ukuaji wa biashara uwe angalau kwa asilimia 20.

Mathuki alitaja miongoni mwa sababu kubwa ya ukuaji mdogo wa biashara kuwa ni pamoja na vikwazo visivyokuwa vya kodi (NBT).

Hata hivyo, alisema taratibu zipo lakini zinawatatanisha wafanyabiashara wa kawaida wadogo wa mipakani, hivyo alishauri serikali za nchi wanachama kutenga bajeti kwa ajili ya kuelimisha jamii.

"Elimu lazima ipelekwe kila kona kuhusu fursa za kibiashara zinazopatikana kupitia wizara zinazohusiana na maeneo muhimu ndani ya jumuiya hiyo," alishauri.

Meneja wa Programu wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ), ambalo linafadhili mradi huo, Dk. Kirstine Focken, alisema tangu kuzinduliwa kwa mradi wa IIDEA miaka mitatu iliyopita, wamesaidia miradi 25 iliyowanufaisha moja kwa moja wafanyabiashara wadogo wa bidhaa na huduma zaidi ya 25,000.

Aidha alisema kuwa wananchi wa Afrika Mashariki zaidi ya 50,000 wamefikiwa kupitia tovuti ya IIDEA huku maonyesho ya masoko na promosheni yapatao 16 yakifanyika katika eneo hilo.

Jumuia hiyo iliyoundwa upya mwaka 1999 na sasa ina nchi sita wanachama ambazo ni Sudan Kusini, Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na Tanzania.

# Wafanyabiashara tanzanite watii agizo

**Na Isack Allan,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA 28, wa madini ya Tanzanite, wamiliki wa migodi na wadau wa madini hayo, wakiwemo wafanyabiashara kutoka Asia waliotakiwa kufika katika ofisi ya Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Simanjiro, wametii agizo la serikali baada ya kuripoti katika ofisi hizo kutoa taarifa ya kiasi cha madini wanayomiliki.

Wadau hao, wafanyabiashara, wamiliki wa migodi na madalali kutoka jijini Arusha wametii agizo hilo, baada ya kufika katika ofisi ya madini Mirerani kutoa taarifa madini wanayomiliki.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, alisema jana kuwa wafanyabiashara wanane walifika ofisini kwa ajili ya kuandika maelezo ya madini waliyonayo.

Alisema kazi ya kuwahoji na kuandika taarifa za wafanyabiashara na wachimbaji wa madini imefanyika kwa muda wa siku tatu mfululizo na anatarajia kukamilisha kazi hiyo mapema iwezekanavyo.

"Leo (jana) na jana (juzi) ofisini walifika wafanyabiashara wanane kati ya 10 tuliopanga kukutana nao kwa ajili ya kuchukua taarifa zao. Kwa wale waliobakia tutaendelea kuwasubiri ili kukamilisha idadi ya watu 28 niliyowataja kufika ofisini kwangu," alisema Ntalima.

Alisema wahusika waliandikiwa barua ya wito huo wakiwamo wale ambao si wanachama wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (Tamida).

Ntalima aliwataka wahusika wote kuhudhuria kufika ofisini kwake ili kutengeneza mahusiano mazuri katika serikali na wafanyabiashara kwa maslahi ya taifa.

Aliwataja wafanyabiashara waliotakiwa kufika ofisini kwake ni Hussein Lemali, Emmanuel Wado (Sunda), Saitoti, Bima, Hamad Mjaluo, Manesh Kotog, Edward Mollel na George Kivuyo.

Wafanyabiashara wengine ni Ben Nkya, Peter Periera, Sam Mollel, Rakesh, Vinal, Reno, Bima, Rajab, Saran, Sailesh, Sidor, Faisal, Hussein Gonga, Jitu, Mula, Shah, Sumil na Frizble.

Oktoba 29, mwaka huu Ntalima alitaja majina ya vigogo walio na madini ya Tanzanite ofisini kwao au nyumbani kufika kwenye ofisini ya madini ili kutoa taarifa za idadi na thamani ya madini wanayomiliki.

## Tamida yawaonya wafanyabiashara

**Allan Isack,** ARUSHA

CHAMA cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (Tamida), kimewataka wafanyabiashara wa madini jijini Arusha, kuzingatia sheria na matakwa ya serikali ya kuhamishia biashara zao katika soko la pamoja la madini lililofunguliwa na serikali jijini hapa.

Mwenyekiti wa Tamida, Sammy Mollel, alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema chama hicho, kinaunga mkono maelekezo ya serikali yaliyotolewa na Waziri wa Madini, Ditto Biteko, wakati akizungumza na wafanyabiashara wakubwa, wadogo na wa kati wa madini hayo, katika soko la madini lililojengwa eneo la Uzunguni jijini hapa. Mollel alisema awali soko hilo lililofunguliwa na Waziri Biteko, Juni 15, mwaka huu, mwitikio umekuwa mdogo kwa wafanyabiashara wa madini kufungua ofisi katika eneo hilo.

Alisema kwa sasa hakuna haja kwa wafanyabiashara hao kukwepa kufanya biashara katika soko hilo, na kuvutana na serikali badala yake wajumuike na wafanyabiashara wengine kulinda maslahi ya soko la madini nchini .

Aidha, Mwenyekiti huyo aliutaka Uongozi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC), kilichopangishia ofisi za madini wafanyabiashara hao, kuongeza kasi ya ujenzi wa ofisi zingine kwa kuwa hadi sasa kuna ofisi 47 wakati mahitaji ni ofisi 100.

Katika hatua nyingine, Mollel amelalamikia tozo ya asilimia moja inayotozwa na serikali kwa mizigo ya madini yanayosafirishwa nje ya nchi (Tasac), pamoja na ucheleweshaji wa vibali jambo linalosababisha biashara hiyo kuwa ngumu. Alisema tangu serikali kuanzisha utaratibu huo, kumekuwapo urasimu wa ucheleweshwaji wa vibali vya kusafirisha madini. Alisema kupata vibali hivyo imekuwa ikichukua siku siku tatu hadi nne jambo ambalo linasababisha baadhi ya wafanyabiashara wa kigeni kushindwa kununua madini hayo.

"Jambo hili linaikosesha serikali mapato ili kupata kibali cha kusafirisha madini ni lazima usubiri siku tatu hadi nne suala hili linasababisha baadhi ya wanunuzi wa kigeni kuondoka bila kununua mzigo," alisema Mollel.

Hata hivyo, aliishukuru serikali kwa jitihada zao za kupunguza baadhi ya matatizo yanayoikabili sekta ya madini hapa nchini.

# Wahudumu kujifunza lugha nyingi za mataifa

**Na Paul William,** MOSHI

BAADHI ya waongoza watalii kwenye Mlima Kilimanjaro wameeleza haja ya kujifunza lugha nyingi zaidi za kigeni ili waweze kuwahudumia watalii kwa weledi.

Aidha, wameeleza kuwa idadi kubwa wanatatizwa na lugha kwa vile wanafahamu zaidi Kiingereza, jambo linalowakwamisha katika mawasiliano na wageni wengine wasiofahamu lugha hiyo wanaokuja nchini kwa shughuli za utalii.

Kutokana na hali hiyo chuo cha Kilimanjaro Information Tachology (KIT), kimetangazwa kuwa kituo cha kujifunza lugha mbalimbali za kigeni ili kumaliza changamoto hiyo katika sekta ya utalii.

Mratibu wa masomo katika chuo hicho Irene Magebo, alisema hayo alipozungumza na Nipashe na kuongeza kuwa waongoza watalii ndiyo waliopewa kipaumbele katika masomo ya kigeni ili kuweza kuimarisha sekta hiyo na kuliingizia taifa na wajasiriamali hao mapato.

"Tutafundisha Kispaniola, Kiitaliano, Kifaransa na Kichina, lengo ni kuwawezesha watakaotoka katika nchi hizo waweze kuhudumiwa ipasavyo "alisema Irene

Mkurugenzi wa chuo hicho, Dk. Alfred Ngowi alisema kutoa mafunzo ya lugha hiyo ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo watoa huduma za kitalii ili kazi zao zifanyike kwa ubunifu na kwa viwango zaidi.

Alisema kwa siku za karibuni kuwekuwa na idadi kubwa ya wageni wasiojua Kiingereza hivyo kushindwa kupata huduma stahiki kama wale wanaoelewa lugha hiyo.

"Hapa tunahakikisha watu wanajifunza hizi lugha ili mwishowe kila mtalii apate huduma stahiki asione kama kuna kubaguliwa na hii ni njia mojawapo ya kukuza utalii wa ndani "alisema

# Wanafunzi sekondari walundikana darasani

**Na Paul William**, MOSHI

SHULE ya Sekondari ya Langasani iliyopo katika kata ya Arusha Chini inakabiliwa na upungufu wa vyumba sita vya madarasa, hali inayowalazimisha wanafunzi kulundikana katika chumba kimoja.

Langasani iliyopo katika Kijiji cha Mikocheni wilayani Moshi, pia inakabiliwa na upungufu wa mabweni mawili.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi, Kastori Msigala, katika taarifa yake ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema kuwa, shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 826 ina vyumba vya madarasa 19 huku uhitaji ukiwa 25.Msigala alisema kuwa, kutokana na changamoto hiyo inayopelekea msongamano mkubwa wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa kunaathiri kujifunza, kufundisha na kufaulu.

Alisema pia kuwa, shule hiyo ni miongoni mwa sekondari ambazo zilipokea fedha za lipa kulingana na matokeo (EP4R), kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kufanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2018 kwa kushika nafasi ya 13 kati ya halmashuri 145 Tanzania Bara na Zanzibar.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa, shule hiyo ilipokea Sh. milioni 121.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili, bweni moja na matundu sita ya vyoo ambapo miradi hiyo inatekelezwa kwa kutumia Force Account.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa madarasa hayo utahusisha kuweka madawati 80 ikiwa ni malengo ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Alisema kuwa, katika ujenzi wa bweni mhandisi wa halmashauri amekadiria kutumika Sh. milioni 140.59 huku fedha zilizotolewa zikiwa milioni 77, ambapo changamoto inayowakabili kwa sasa ni kutokamilika kwa bweni hilo kutokana na sababu na kutotosheleza kwa kiwango cha fedha kilichopo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa, zipo baadhi ya changamoto ambazo wamekumbana nazo kuchelewesha kuletwa ramani za majengo baada ya fedha kuingizwa katika akaunti ya shule pamoja na tatizo la fedha kuchelewa kusomeka katika mifumo ya FFARS.

"Changamoto nyingine ni vifaa vya ujenzi kutopatikana katika maeneo ya jirani na mradi hali iliyosababisha kazi ya kuvisafirisha kuwa mgumu na kufanya gharama kuongezeka" alisema Msigala.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Atashasta Nditiye (wa pili kulia) akifurahia jambo na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mgwira, wakati wa hafla ya uzinduzi wa safari ya ndege ya Shirika la Ndege la Uganda kutoka Entebbe kwenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), juzi. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Wengi zaidi wapata maji

**Na Paul William,** HAI

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 4.1 kufanikisha miradi mikubwa kwa midogo ya maji katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Hatua, hiyo imefanikisha upatikanaji wa maji kutoka asilimia 85 kwa mwaka 2015 na kufikia asilimia 87 mwaka huu (2019).

Lengai ole Sabaya, Mkuu wa Wilaya ya Hai, alibinisha hayo wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/20 kwa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi mkoa wa Kilimanjaro.

Sabaya alisema kuwa, katika kipindi cha miaka minne tangu serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani huduma mbalimbali za kijamii katika wilaya hiyo zimeboreshwa lengo likiwa ni kuwahudumia wananchi kwa ukaribu zaidi pamoja na kuwatatulia matatizo yanayowakabili.

Alisema kuwa, katika sekta ya afya kiasi cha Sh. milioni 267.95 zimechangwa na vyama vya ushirika kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha afya katika kata ya Weruweru ikiwa ni jitihada za serikali ya wilaya kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuhamasisha wadau kuchangia maendeleo.

Mkuu huyo wa wilaya alieleza kuwa Sh. bilioni 1.72 zimetolewa na serikali kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba pamoja na vitendanishi hali ambayo imepelea wananchi kupata huduma za dawa kwa ukaribu zaidi.

Katika sekta ya elimu bila malipo kiasi cha Sh. bilioni 6.5 zimetolewa na serikali ambapo katika elimu msingi zimepelekwa takribani bilioni 1.9 huku elimu sekondari ikipelekwa bilioni 4.6.

Sabaya akizungumzia uboreshaji wa miundombinu ya shule alisema Sh. milioni 454.18 zilitolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule ikiwamo ukamilishaji wa ujenzi wa maabara mbili, madarasa na matengenezo ya vitanda 30 Sekondari ya Harambee.

"Pia katika fedha hizo za uboreshaji wa miundombinu zipo pesa za ukamilishaji wa vyumba 11 vya madarasa katika shule saba pamoja na ufuatiliaji wa mradi, ukusanyaji wa takwimu na uhamisho wa walimu" alisema Sabaya.

Aliongeza kuwa, katika sekta ya kilimo Sh. milioni 844 zilipokelewa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa mifereji kwa ajili ya umwagiliaji na kuweza kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 966 hadi hekta 10,266.





Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. David Mwamfupe (aliyevaa suti), akiwaongoza wabunge kutoka nchi ya Kenya, wakati walipofanya ziara ya kujifunza na kuona ujenzi wa majengo mbalimbali, ikiwamo stendi kuu ya mabasi, unaoendelea katika eneo la Nzuguni Nanenane, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wabunge Kenya wataka Afrika kumuiga JPM

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WABUNGE wa Kamati za Majimbo kutoka Kenya wamezishauri nchi za Afrika kuiga mfano wa kasi ya maendeleo na uaminifu wa matumizi ya fedha za umma unaofanywa na Rais John Magufuli.

Wabunge hao walisema hayo kwa nyakati tofauti walipokuwa kwenye ziara ya kukagua na kujifunza miradi inayosimamiwa na jiji la Dodoma kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa makao makuu ya serikali

Mbunge wa jimbo la Mjini, Fred Kapondi, alisema kuwa nchi za Afrika zinatakiwa kuiga mfano wa kasi ya maendeleo katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali inayofanywa na Rais Magufuli kwa ajili ya Watanzania.

Alisema Rais wa Tanzania ameonyesha uaminifu katika matumizi ya fedha za umma zinazotolewa kwa ajili ya kuleta maendeleo mbalimbali nchini ikiwamo ujenzi wa miundombinu kwa upande ya makao makuu ya serikali.

"Tanzania chini ya uongozi wa Rais Magufuli kwa kweli imeonyesha uaminifu kwenye matumizi ya fedha za serikali zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ukilinganisha na nchi nyingine nyingi za Afrika," alisema.

Mbunge Jenithe Tiney, alisema katika ziara hiyo wamejifunza jinsi serikali inavyotekeleza miradi yake ya maendeleo kwa uaminifu wa hali ya juu kwa ajili ya kuwanufaisha raia wake.

Tiney, alisema kuwa katika ziara hiyo wameona miradi ya mabilioni ya fedha ambayo anaamini itawaletea Watanzania maendeleo makubwa bila kujali itikadi za kisiasa na kidini.

"Hakika kila hela inatumika inavyotàkiwa na ndiyo maana miradi hiyo ya kisasa inaonekana kwa vitendo,"alisema.

Kwa upande wake Meya wa jiji la Dodoma, Prof. David Mwamfupe, akizungumza kwenye miradi ya soko kuu na stend kuu ya mabasi alisema hadi kufika Disemba mwaka huu itakuwa imekamilika na kujiendesha yenyewe.

# Waagizwa kufika polisi kuhojiwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKATI mradi wa ujenzi wa zahanati ya mtaa wa Zepisa jijini Dodoma ukisuasua kwa zaidi ya miaka tisa, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ametoa siku 90, kwa wahusika kuukamilisha.

Akizungumza wakati wa mkutano baina ya wananchi wa Zepisa na viongozi wa jiji Katambi aliwaagiza wajumbe wote wa kamati ya ujenzi wa zahanati hiyo kuripoti kituo Kikuu cha Polisi Jumatatu Novemba 18 mwaka.

Aidha, aliwataka kufika kwa ajili ya mahojiano kufuatia kuwapo viashiria vya ubadhirifu wa fedha za mradi huo.

Halikadhalika, aliagiza kuwa ndani ya muda huo,Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, awe amepeleka walimu katika Shule ya Msingi Zepisa inayokabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu na vyoo. Alisema shule hiyo yenye wanafunzi 1,002 ina walimu sita kati ya hao watatu hawapo kituoni kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo baadhi yao kutolipwa fedha za uhamisho.

Akitoa maagizo hayo kwenye mkutano huo wa hadhara wa kijiji hiko ikiwa ni muda mfupi baada kufanya ziara ya ukaguzi kufuatia malalamiko ya wananchi, alisema haiwezekani fedha za ujenzi zitolewe halafu kazi isuesue.

"Haiwezekani ujenzi wa zahanati uchukue miaka tisa wakati Rais John Magufuli ana muda miaka minne madarakani, lakini kajenga hospitali za wilaya na vituo vya afya kila kona ya nchini," alisema Katambi.

"Nahitaji kuona huduma za zahanati zinaanza mara moja staki kusikia habari zenu za kulumbana isipokuwa kazi ikamikike," aliagiza Katambi. Akizungumzia suala ya ujenzi wa vyoo, Mkuu wa Wilaya alisema ndani ya mwezi mmoja viwe vimekamilika ili wanafunzi waanze kuvitumia.

Alisema vyoo vilivyopo ni vya muda mrefu na vimechakaa na kwamba vinahitajika kujengwa upya kwa sababu vina mazingira hatarishi kwa usalama wa wanafunzi. "Mkurugenzi wananchi wamejitolea kuchimba mashimo na nguvu yao imefikia hapo. Sasa unatakiwa kuvikamilisha na kama nilivyoagiza ndani ya mwezi mmoja muwe mmemaliza pia kuleta walimu hapa", alisema Katambi.

Alisema shule hiyo imekuwa ikitumia vyoo vilivyojengwa mwaka 1978 hali ambayo inasababisha wanafunzi kukosa utulivu wa kujifunza na kuwa na matokeo mabovu.

Kwa upande wa mwakilishi wa Mkurugenzi Shaban Juma, alisema mradi huo ulisuasua kutokana na malumbano yaliyojitokeza kati ya uongozi wa kijiji, kata na kamati ya ujenzi.

Hata hivyo alisema wamepokea maagizo ya Mkuu wa Wilaya na ndani ya muda huo ujenzi wa zahanati hiyo utakuwa umekamilika na wananchi wataanza kupata huduma.

Diwani wa Kata ya Hombolo Makulu, Lemanya, alisema licha ya taratibu zote kufuatwa kulikuwa na ukwamishaji wa makusudi wa taratibu.

# Atoa maagizo ya umeme Chamwino

**Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dokta Medard Kalemani,

ameiagiza Tanesco Mkoa wa Dodoma kuanzia wiki ijayo kupeleka umeme katika vitongoji vyote vya kata ya Mlowa wilayani Chamwino.

Alisema hatua hiyo inalenga ili kuinua uchumi wa wananchi wanaofanya biashara mbalimbali na uwekezaji.

Kalemani alitoa kauli hiyo juzi wakati akiwasha umeme katika hospitali ya Wilaya ya Chamwino mkoani hapa, ikiwa ni muendelezo wa kuunganisha nishati hiyo katika vijiji na kata zote za eneo hilo.

Waziri alisema lengo la serikali ni kwamba kufikia Juni 2020, jimbo lote la Mtera litakuwa na umeme na kazi ya kupeleka kwenye vitongoji itaendelea hadi ifikapo Juni, 2021.

"Vijiji 38 ndani ya miaka minne vinaumeme na leo vijiji viwili vinakwenda kuuwasha vitafikia 40, tunapaswa kuipongeza serikali ya awamu ya tano kwa jitihada inayoifanya katika sekta ya nishati," alisema Dk. Kalemani.

"Rais John Magufuli ametoa fedha nyingi, zaidi ya bilioni 36 kuwaletea umeme Mkoa wa Dodoma. Ni wajibu wenu kuchangamkia kuunganisha umeme nitakuja kukagua kuona mmefikia wapi,"alisema Waziri.

Alifafanua kuwa vijiji 20, vilivyobaki vipo kwenye mpango lakini vinne kati ya 20, vinaanza kupelekewa umeme wiki ijayo na Tanesco.

"Vijiji vingine 16 vinavyobakia vitapelekewa umeme Februari mwaka 2020 ambapo tutakuwa tumekamilisha vijiji 60, vya jimbo la Mtera"aliwaambia.

Aidha aliionya Tanesco kuwatoza wananchi gharama kubwa ya kuunganisha umeme akisema isizidi Sh.27, 000 ambazo zimepangwa na serikali.

"Msijaribu kuzidisha gharama ya kuunganisha umeme iwe mkandarasi, Tanesco mwenyewe au REA, atakayefanya hivyo nakuagiza Meneja nikute umemfukuza kazi usipomfukuza nakufukuza wewe,"alisema Dk.Kalemani.

Kwa upande wake, Meneja Tanesco Wilaya ya Chamwino Baltazar Massawe, alisema umeme huo utawawezesha wananchi kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwamo wanafunzi na walimu kusoma na kufundisha.

Alisema kuwashwa umeme pia ni kuboresha huduma za afya , aidha kwa wananchi wataanzisha viwanda vidogo vidogo vya uzalishaji bidhaa.

Mbunge wa Mtera, Livingstone Lusinde, alisema alimuomba Waziri Kalemani kufikisha umeme katika hospitali hiyo ili kurahisisha huduma za kiutendaji.

"Nakushukuru Waziri baada ya kusikia kilio chetu cha umeme, kuna baadhi ya maeneo yamerukwa, nikuombe sana ujio wako kwa mara nyingine tupate umeme katika kitongoji cha Sokoine ambacho kuna mradi wa maji. Lakini niseme pale hakuna umeme na pia haupo kwenye makanisa na misikiti,"alisema Lusinde.







Balozi wa bidhaa za Emina, Miriam Mauki (katikati), akikata utepe kuzindua Tuzo za Wapishi za Emina, chini ya kampeni ya Mbabe wa Usafi, zinazoendeshwa na kiwanda cha Bingwa Laboratories Ltd, jijini Dar es Salaam jana, zenye lengo la kutoa zawadi mbalimbali, semina na mafunzo, kwa Baba na Mamalishe nchini. Wa (tatu kulia) ni Katibu Mkuu wa Baba na Mamalishe Mkoa wa Dar es Salaam, Ally Luyaya na Mamalishe kutoka soko la Magomeni, Hellen Mwita. **PICHA: JOHN BADI**

# Zanzibar yahimiza kuwa na viwango vya matofali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TASISI ya Viwango Zanzibar (ZBS), imetakiwa kuanzia sasa kudhibiti kikamilifu viwango vya ubora wa vifaa vinavyotumika katika sekta ya ujenzi wa makazi na majengo ya biashara.

Jukumu hilo likifanyika litawawezesha wananchi kuepukana na majanga yanayoweza kujitokeza baada ya makazi yao kukamilika.

Mwenyekiti wa Bodi ya ZBS, Khamisa Mkanga, aliyasema hayo wakati akifungua semina juu ya namna bora ya kutengeneza matofali kwa wafanyabiasha hiyo, iliyofanyika Kikwajuni Zanzibar. Alisema leo Zanzibar kuna majengo mengi ya kisasa lakini yanatakiwa kutazamwa katika hali ya kiwango ili yasije kuleta maafa baadaye.

Alisema ZBS imeamua kufanya mkutano na wamiliki wa vituo vya utengenezaji matofali ili kuwa na uhakika matofali yanayotengenezwa yana ubora unaotakiwa.

Alieleza kuwa katika kuhakikisha kuwa kila kitu kinakuwa na ubora katika utengenezaji huo wa matofali, ZBS itayachukuwa maoni ya wafanyabiashara hao ili kuelekeza namna ya kupanga mipango imara .

Mkurugenzi wa ZBS Khatibu Mwadini Khatib, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuvichunguza na kuvifanyia kazi vifaa vya ujenzi ili kujua kama vina ubora wa kuvitumia.

Alieleza kuwa tasisi hiyo imekuwa ikisimamia ubora wa vitu mbali mbali ili kuhakikisha bidhaa hizo zinatumika kwa manufaa ya wananchi bila ya kuwa na athari yoyote.

Alisema katika kuhakikisha kuwa ujenzi unakuwa na ubora, lazima wauza matofali kufanya biashara yenye ubora kwa kuwauzia wananchi bidhaa bora.

Kwa upande wake Meneja Mwandamizi wa kampuni ya saruji ya Twiga ya Dar es Salaam, Danfor Samwenda, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia ubora wa matofali ili kuepusha madhara kwa wananchi .

Alisema hivi sasa Tanzania inazalisha sementi yenye ubora hivyo wafanyabiashara hao wanatakiwa kuitumia kuliko kuagiza biashara kutoka nje ya nchi.

# SMZ yapongeza wafanyabiashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, amesema serikali inatambua na kuthamini mchango wa wafanyabiashara kwenye kuendeleza na kukuza uchumi wa nchi.

Aliyasema hayo ofisini kwake Mjini Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari jana.

Alieleza kuwa mchango wa wafanyabiashara Zanzibar, umekuwa mkubwa kwani uwepo wao umewawezesha wananchi kupata mahitaji yao pamoja na kuongeza mapato yao na ya taifa.

Aidha, aliwaambia kuwa serikali imekuwa ikiweka mazingira bora kwa wafanyabiashara na kuona wanafanya shughuli zao bila ya usumbufu.

Akizungumzia mazingira hayo, alisema ni pamoja na kuimarisha bandari na miundombinu mingine ambayo itawawezesha kufanya biashara zao bila ya kubughudhiwa na yeyote.

"Serikali inawajali sana wafanyabiashara wake ikiwa wanafuata sheria na utaratibu uliowekwa kwani kwani ni miongoni mwa wadau wakubwa katika kuongeza mapato ambayo yanatumika katika maendeleo mbalimbali," alisema.

Naibu Waziri huyo alieleza kuwa wapo baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakienda kinyume na sheria za nchi ikiwamo kuingiza vyakula vibovu na vilivyopitwa na muda hali ambayo ni hatari kwa afya za wananchi.

"Wapo baadhi wanakiuka sheria kwa kununua bidhaa ambazo hazina viwango na kuja kuuzia wananchi, hili hatutalikubali hata kidogo,"alisema.

Alieleza kuwa, mfanyabiashara yeyote atakayekamatwa na bidhaa iliyokuwa haina kiwango atachukuliwa hatua ikiwamo bidhaa zake kuharibiwa.

Alisema lengo la serikali ni kuona wananchi wanakula vyakula vyenye ubora kwa ajili ya kuimarisha afya zao na sio kula vyakula ambavyo si salama vinavyowadhuru.

Naibu Waziri, aliwashauri wananchi kuacha kununua vyakula vilivyopita muda wa matumizi kwani ni hatari kwa matumizi ya afya zao.

# Waambiwa fursa zipo kwenye utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imewataka vijana wa Zanzibar kutumia majukwaa ambayo yanatoa fursa za ajira kupitia sekta ya utalii ili kujikwamua na umaskini.

Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, aliyasema hayo katika mdahalo wa maendeleo endelevu ya utalii na nafasi ya uongozi kwa vijana.

Alieleza kuwa ikiwa vijana wanatafuta taarifa za utalii wataweza kuingia katika ushindani wa soko la ajira.

Aliwaambia kuwa vijana wengi wanalalamika kukosa taarifa sahihi za utalii na soko lake kutokana na kutofuatilia kwa usahihi habari hizo.

Waziri huyo alisema Zanzibar kuna fusa nyingi za ajira lakini zimekuwa zikichukuliwa na wenzao wanaotoka nje ya Zanzibar kutokana na Wazanzibari kutochangamkia fursa hizo.

"Zaidi ya vijana 100,000 wanaotoka nje ya Zanzibar wanakuja kuchukua fursa za ajira hapa kwetu kutokana na kuzifatilia na kuzichukua. Inasikitisha kuona kijana aliyekuwapo hapa fursa hii haimfikii wala kuisikia," alisema Waziri Kombo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeunda mabaraza ya vijana na kutoa Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kuwawezesha kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Alidha, aliwataka vijana kufatilia fursa za utalii kwa maendeleo yao badala ya kulalamika kuwa hawana ajira.

Kwa upande wake mshauri wa maendeleo ya vijana Mustafa Sharif, alisema ili kufikia maendeleo endelevu ya utalii ni lazima mwananchi ajue thamani ya utalii.

Aidha aliwaambia kuwa Zanzibar ni sehemu moja ambayo ina utalii mkubwa hivyo ni vyema kutumia fursa hiyo ambayo itamuwezesha kujiajiri na kupata kipato.

Kombo alisema ni vyema kwa serikali kuhakikisha kwamba mazuri ya sekta ya utalii yanazungumzwa ili yaweze kujulikana na kuvutia wageni wanaoingia nchini.

"Zanzibar ina historia kubwa ikiwamo magofu, fukwe na sehemu nzuri ya kihistoria ya Mji Mkongwe ambao upo katika urithi wa dunia hadithi kama hizi zikitolewa na kuzunguka wananchi wataweza kuzisikia na kujua thamani ya utalii wao," alisema.

"Tunajua kwamba utalii tuliokuwa nao upo katika soko la ushindani ikiwamo nafasi za kazi zilizokuwa bora ambazo zinashindaniwa katika soko hilo kupitia nchi mbalimbali ikiwamo Kenya,Uganda, Ruwanda na nchi nyengine za Afrika Mashariki,"alisema.

Alisema imefika wakati kwa vyuo vilivyokuwapo Zanzibar kubadilisha aina ya mtaala uliokuwepo wa masuala ya utalii kwa kufundisha kinadharia na kivitendo ili kumpa uwezo mwanafunzi kupata stadi ambazo zitamuwezesha kuingia katika soko la ushindani.

Mshiriki wa mdahalo huo Ahlam Hassan Omar ambaye ni mwanafunzi wa sekta ya utalii aliwashauri vijana hasa wa kike kuulinda na kuendeleza utalii wao kwa maslahi yao na vizazi vijavyo.

Alitumia fursa hiyo kuwaomba viongozi kuendelea kuwapa elimu wananchi hasa vijana wa kike kuhusu maendeleo ya utalii ili kuijenga nchi kwa misingi ya maendeleo endelevu kiutalii na kuleta mabadiliko ya kiuchumi.



KIBA Soma UK.16

# BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI NOVEMBA 16, 2019



# MUNGU ANAKUONA

## UNA MKE NA MCHEPUKO, UNALALA KWA MLUPO!

Soma UK.15

## BASI SAWA



## Uwoya azidisha utata ujauzito wake

MWIGIZAJI mkongwe Irene Uwoya, amefunguka akisema anamshukuru Mungu kama watu wanamtabiria kuwa mjamazito kwani yeye ni mwanamke na ana hamu ya kupata mtoto.

"Inshallah kama wanasema nina ujauzito, Mungu ndiye anayejua hata mimi natamani kupata mtoto," amesema Uwoya.

Wiki hii kumeibuka tetesi kwamba msanii huyo ana ujauzito na picha yake inayoonesha akiwa katika hali hiyo ikisambaa kwa kasi kwenye mitandao ya kijamii.




## Hemed PHD hodari kwa kujipenda

MSANII wa Bongo Muvi, Hemedy PHD, amesema anajipenda mwenyewe kuliko mwanamke na kwamba anatumia muda mwingi kujipamba.

Akizungumza na EATV, alisema kuwa sababu ya kuzaliwa mzuri 'Handsome Boy' ni kutokana na mama yake kujifungua huku akiwa anakunywa kinywaji.

Hemedy PHD amesema wale wanaosema kwamba yeye anapenda sana wanawake wanakosea kwani kila wakati anajiweka namba moja kabla ya kumfikiria mtu mwingine.

"Hapana sipendi wanawake, najipenda mimi mwenyewe tena najipenda sana kuliko kitu chochote na upendo unaanza na mimi kwanza. Watu wanaongea sana na kila mtu anaongea lake si unajua tena ukizaliwa 'handsome boy', mimi Mama yangu amenizaa anakunywa kinywaji kwa hiyo ndiyo maana nimetokea hivi mauzo mengi.", amesema Hemedy PHD.



# MJOMBA FUJO ' AMCHAMBUA MAGUFULI

MSANII wa nyimbo 'kughani', George Paul Mzelu, maarufu kama 'Mjomba Fujo', ametoka na wimbo maalum uliochambua ufanisi wa utawala wa rais John Pombe Magufuli.

Wimbo huo unaojulikana kwa jina la ' Huyu ndiye Magufuli', amemshirikisha pia msanii wa muziki wa kizazi kipya, Amini Mwinyimkuu (Amini) na tayari umeshaanza kusikika kupitia vituo mbalimbali vya radio, luninga na katika mitandao ya kijamii.

Akizungumzia wimbo huo, msanii huyo, ambaye kwasasa anatamba na wimbo wake wa kwanza wa 'Kesho' alisema, mafanikio ya Awamu ya Tano ndiyo yalimfanya atunge wimbo huo kama njia ya kumpongeza.

Alisema wazo la kutunga wimbo huo ulitokana na ukweli kuwa, tangu kuanza kwa awamu ya tano ya Rais John Magufuli kuna mambo mengi yamefanikiwa kwa mujibu wa matarajio ya Watanzania walio wengi ambao ni wanyonge.

"Nimeangalia kila mafanikio ya awamu ya tano, ndipo nikaamua kuketi chini na kuanza kuhesabu utendaji wa serikali, nikapata mashairi ya wimbo huu, 'Huyu ndiye Magufuli".


Aliongeza "Kama walivyoonena Wahenga ya kwamba 'Kila Chanda chema lazima kivikwe pete' huu ni wimbo uliochambua na kutanabaisha kila nyanja na matunda yaliyopatikana, ndiyo maana sikupata tabu ya kumwagia sifa ambazo zinamstahili Rais huyu wa Awamu ya Tano ". alisema Mjomba Fujo.

## INSTA-TWITTER





**Hii** ni baada ya yule dada na mshika pochi wake kuharibu hali ya hewa, tamko soon linakuja-**Yusuph Mlela.**



**Ni** mwendo wa mangumi plus. Nimeskia kuna mtu anataka kunipiga-**Ebitoke.**




## Kadinda amweka nyuma Wema

MBUNIFU wa mavazi nchini, Martin Kadinda, amesema kazi ngumu ya kuendesha biashara zake zimesababisha kuwa mbali na Wema Sepetu.

Martin Kadinda ameiambia EATV, si kweli ukaribu wao wa mwanzo umepungua bali inatokana na kila mtu kwa bize na kazi zake.

"Hayo ni mawazo binafsi ukiangalia kwenye mitandao ya kijamii nipo na Wema Sepetu, mimi mwenyewe nilikuwa naye kwangu. Nimeamua kumuweka Wema nyuma sio mbele kama ilivyokuwa mwanzo kwa sababu mimi nina biashara natakiwa kuifanya na yeye anatakiwa aendeleze maisha yake" amesema Martin Kadinda.



# MUNGU ANAKUONA

## UNA MKE NA MCHEPUKO, UNALALA KWA MLUPO!

RAPA Nay wa Mitego, amepakua kazi yake mpya inayoitwa 'Mungu Anakuona' ambayo tangu ilipotambulishwa siku tatu imekuwa gumzo la jiji.

Ndani ya wimbo huo, mwanamuziki huyo ametumia maneno yanayofanana na yale ya kifalsafa akikemea vitendo vinavyofanywa kinyume na watu kutoka jamii zote. Ndani ya wimbo huo, Nay amewaonya viongozi wa dini, wazinzi, washirikina na mambo mengine huku akiwaambia Mungu anawaona.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Huwa** najisuka mistari mwenyewe nyumbani, ila leo nimezingatia zaidi ili hata nikikutana na Ebitoke mambo yakiharibika huko ndani pawe panaeleweka-**Lady Jaydee.**



**Wengine** tuache kushobokea mapenzi maana tutazikwa wazima wazima-**Amber Lulu.**



**Haya** ni maamuzi yangu. Basi mtachangia hoja hata hamjui ni nini!!-**Aunt Ezekiel.**

# Kuumbe!



# UNFORGETTABLE TOUR

## ALI KIBA KUWASHIKA MIKONO MASHABIKI WAKE

MFALME wa Bongo Fleva, Alikiba, ametangaza ziara yake ya muziki ambayo itaegemea zaidi burudani, afya, jamii na michezo.

Ziara hiyo aliyoipa jina la Unforgettable Tour, itaanzia mkoani Mwanza siku ya Novemba 29 na kuambatana na shughuli mbalimbali za kijamii.

Akizungumza na EATV amesema katika ziara hiyo watakuwapo na wasanii wengine ambao atawatangaza baada ya kuona wana vigezo vinavyokubalika.

Amesema amechagua Mkoa wa Mwanza kuanza kwa ziara yake kutokana na hamu yake ya kuona anafurahia pamoja na wakazi wa jiji hilo kutokana na kumshika mikono siku zote.

"Nilikuwa nataka nikasheherekee birthday yangu, Mwanza ni watu wangu ambao walikuwa wananipa sapoti siku zote, nikifanyaga shoo vilevile ni mji mzuri sana na mkubwa," amesema

Akizungumzia vigezo vya msanii kupata nafasi ya kuwapo kwenye tamasha lake.

Alitaja baadhi ya vigezo ni wale wale wasanii ambao amefanya naye kazi pamoja na wale ambao watatambulisha nyimbo "Live".

"Kuna wasanii wenzangu ambao wangependa kufanya kazi na mimi siku zote huwa wananisapoti, kwahiyo ratiba itabadilika", ameongeza.

Pia Ali Kiba amesema kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa 'sapraizi' ya nguvu ya msanii yeyote kutoka nje ya nchi.



# Wapiga tumba wanavyonogesha muziki

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE muziki hasa wa dansi kuna chombo kinaitwa tumba au konga.

Hizi ni ngoma mbili au tatu ambazo huchanganywa na vyombo vingine kama magita, drums, kinanda, trumpet, saxaphone na vingine ambavyo vikipangiliwa kwa pamoja hutoa mirindimo inayovutia.

Kwa wale wasiojua tumba zile ngoma ambazo Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli huwa anazipiga wakati anapokuwa mgeni rasmi kama kuna bendi ya dansi ikitumbuiza.

Rais Magufuli naye ni mahiri mno kwenye chombo hicho cha muziki.

Kiasili tumba ni ngoma za kawaida tu kama zile za kiasili, ila zile zinazoonekana kwenye bendi ziko za aina mbili. Kuna zingine ni ngozi ya wanyama, lakini zingine zimetengezwa kiwandani kwa kutumia vitu kama ngozi au plastiki laini, lakini mlio wake ni kama ngoma za kawaida.

Kazi yake ni kuweka vionjo ili muziki uvitie zaidi hasa kwa muziki wenye mahadhi ya kiafrika.

Tanzania imepata kuwa na bahati ya wapiga tumba waliokuwa na uwezo mkubwa wa kuzikung'uta na kufanya burudani tosha kwa mashabiki.

Leo tunawaangalia wapiga tumba waliotamba wakiwa na bendi mbalimbali nchini.

### CD Morris

Ni mmoja wa wapiga tumba mahiri ambao Tanzania ilibahatika kuwa nao. Alitamba sana kuanzia katikati ya miaka ya '70 hadi mwanzoni mwa miaka ya '90 alipofariki dunia.

CD Morris, alianzia na Safari Trippers na kuzunguka bendi mbalimbali, ikiwemo Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma', 'Maquiz Du Zaire' na hadi anafariki dunia alikuwa kwenye bendi ya MK Group.

Ukizisikiliza nyimbo ambazo amepiga tumba, utagundua kuwa alikuwa na kipaji cha aina yake, kwani anavyozipiga unaweza ukadhani ni iliyopiga ni mashine na si mikono ya mwanadamu.

Pia alikuwa na mbwembwe jukwaani kiasi cha mashabiki kumzunguka na kumkodolea macho kwa mshangao badala ya kucheza muziki.

### Ally Jamwaka

Inabidi Tanzania ijivunie kuwa na mwanamuziki kama huyu, kwani ni mmoja wa wapiga tumba wachache mahiri ambao bado wako hai.

Ally Jamwaka, ana uwezo mkubwa wa kutumia tumba na wakati mwingine akipiga utazisikia zikisikika wazi kana kwamba ngoma ya mdundiko hivi.

Kwa kipindi kirefu cha maisha yake ya muziki amepigia DDC Mlimani Park Orchestra ambayo alianza nayo hadi leo hii yupo.

Hata hivyo alishawahi kutoka kwa kufanya kazi kwenye bendi kadhaa, ikiwamo Vijana Jazz Band.

### Mohamed Chomachoma

Hata bahati tu kujulikana au kupata sifa kwa mashabiki wa muziki, lakini wanaohudhuria bendi mbalimbali wanamfahamu mwanamuziki huyu kuwa ni mmoja wa wakung'uta tumba kwenye kiwango cha hali ya juu, pamoja na machachari yake jukwaani hufanya muziki uchangamke kupita kiasi.

Mohamed Chomachoma alipachikwa jina la 'mikono ya tembo' na hayati Tx Moshi William alipokuwa na bendi ya Msondo Ngoma. Mbali na Msondo, kipaji chake kilianza kuonekana kwenye bendi ya Diamond Sound Wana Dar es Salaam Kibindankoi, Dar Mosica na FM Academia.

Mwaka jana alikuwa kwenye bendi ya Ya Capital Wazee Sugu inayoongozwa na Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki.

### Mohamed Haroub

Alikuwa mpiga tumba mahiri wa bendi ya Uda Jazz kiasi cha bendi kubwa kama Juwata Jazz kumchukua kwenye miaka ya '80.

Haroub ambaye ni marehemu kwa kiasi kikubwa ndiye aliyepiga nyimbo nyingi kuanzia miaka ya '80 hadi mwishoni mwa miaka hiyo.

### MCD

Kwa kizazi cha miaka ya hivi karibuni watamkumbuka mpiga tumba huyu mahiri, aliyekuwa akipiga kwa mbwembwe huku mdomoni akiwa na filimbi.

MCD alijipatia umaarufu wake kwenye bendi ya African Stars, 'Twanga Pepeta' mwanzoni mwa miaka ya 2000 ambapo alipiga chombo hicho karibuni nyimbo zote maarufu kama 'Kisa Cha Mpemba', 'Kuolewa', 'Busu la Kufunga Mwaka' na nyingine nyingi.

Kabla ya kifo chake kwenye hospitali ya KCMC Moshi mwaka 2014, aliwahi pia kupigia bendi ya Mashujaa Musica.



# Vijimambo


1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Pretty Girl
## Bora kidonda kuliko kovu la mapenzi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine tabia ya mtu inatokana na sehemu aliyotokea, mazingira yaliyomzunguka au tukio lililomtokea zamani na kumuathiri kisaikolojia.

Unaweza ukakutana na mwanamume ambaye hataki kabisa wanawake, au hataki kuoa, kumbe huko nyuma alishawahi kukutana na maswahiba ya kutendwa, ya kukimbiwa na mwenza wake.

Hata wanawake ni hivyo hivyo, Unamkuta hataki mwanamume au kuolewa. Matukio haya yanawafanya kuona mwanamume au mwanamke yoyote anayemuona kuona ni wale wale tu na anaweza kufanyiwa vile vile tu kama mwanzo. Hii imewaathiri wengi kwenye jamii.

Mtunzi wa filamu ya 'Pretty Girl' ana mtazamo huo. Ni filamu iliyochezwa na Vicent Kigosi maarufu kama Ray, Mohamed Mwikongi maarufu kama Frank, Hashim Kambi, Hassan Moshi au Tx Junior, Salma Jabu 'Nisha', Irene Uwoya, Tino Muya na wengineo.

Irene ni bosi kwenye kampuni moja hivi. Lakini pamoja na kuwa mwanamke ambao wengi wao wana huruma, lakini amekuwa na tania ya ukali, akinyanyasa wafanyakazi wake, hasa wa kiume.

Baada ya muda mrefu, ukali wake unasababisha kampuni kuanza kufilisika taratibu kutokana na uongozi mbovu.

Ray, kijana tajiri, anaamua kuwekeza kwa kununua hisa na kuifanya kampuni kuinuka upya.

Hata hivyo bosi anaendelea kuwa yule yule Irene.

Bodi ya Wakurugenzi inakutana kwa nia ya kutatuta tatizo. Baada ya majadiliano inagundulika kuwa bila Irene kuondoka, kampuni hiyo itaendelea kufilisika au kulegalega.

Ray na jopo lake la wakurugenzi wanajadili tatizo la Irene na kugundua kuwa ameathirika kisaikolojia.

Anatafutwa daktari kwa ajili ya kutatua tatizo lake, lakini mwenyewe anapinga na kusema kuwa hana jambo lolote linalomsibu na wala haumwi.

Kampuni sasa inamlazimisha kwa nguvu afanye hivyo, naye anakubali kwa shingo upande.

Huko kliniki, baada ya maswali kwa siku kadhaa, hatimaye inagundulika kuwa ni kweli alikuwa na matatizo yaliyotokana na ukatili kutoka kwa mumewe hapo zamani.

Ilianza kwa kulazimishwa na wazazi wake kuolewa na mwanamume asiyempenda. Kumbe wakati yeye hampendi na mwanamume pia alikuwa hakuwa anampenda. Mume akawa anamchukulia poa mkewe.

Ndani ikawa tafrani. Akawa anamletea mkewe wanawake wengine ndani. Irene anapokwenda kwa wazazi wake anarudishwa kwa mumewe.

Hali ilikuwa mbaya zaidi mume alipomkodishia vijana wa kihuni ili wambake kwa sababu hampendi na hataki kuondoka.

Irene akamwambia daktari kuwa hiyo ndiyo sababu iliyomfanya awe na tabia hiyo ya kuwa mkali na kuwachukia ovyo wanaume.

Pamoja na yote hayo, kijana tajiri mwenye hisa nyingi kwenye kampuni hiyo, Ray anamwambia Irene afute historia yote ya nyuma, kwani tangu alipomuona kwa mara ya kwanza alitokea kumpenda kwa dhati na anataka kumuoa, ili kumfanya awe mtu mpya na



# NANI HAMTAKI?

## DRAKE AWAAMBIA ZOMEENI YEYE YUPO TU

AMA kweli mkubwa anapojikwaa husingizia kuna wageni! Ndivyo yaliyomkuta rapa mkubwa wa Marekani, Drake, baada ya kujikuta akizomewa na mashabiki wakati akitumbuiza.

Lakini pamoja na tukio hilo la kushangaza, bado Drake amekaza moyo na kueleza tukio hilo ni kama kumkaribisha mgeni kwani mashabiki wa aina hiyo atakutana nao kila mwaka.

Tukio hilo lilikuwaje? Mkasa mzima ulitokea usiku wa Jumapili wakati wa kuanza Tamasha la Camp Flog Gnaw Los Angeles kwa mara ya kwanza ambalo limenzishwa na Tyler, na ilitangaza kutakuwa na msanii mkubwa mwalikwa atakayetumbuiza.

Mashabiki walizingatia tangazo hilo na ndipo swali likawajia nani atatokea msanii kinara atakayetumbuiza? Lakini baadhi yao walijiongeza wakiwa na uhakika wa kumuona Frank Ocean akipanda jukwaani na Jina lake ndio wote walikuwa wanalitaja uwanjani hapo.

|Jambo la kushangaza wakati alipokaribishwa msanii kinara, ghafla aliibuka Drake kitu ambacho kilionyesha watu hawakufurahishwa nacho na hapo ndipo zilizuka kelele za kumzomea hadi kupelekea msanii huyo kushuka juu ya ukwaa.

Baada ya tukio hilo, Drake amejitokeza na kusema kama watu hao hawamtaki katika tamasha hilo la Camp Flog Gnaw, basi watakuwa kama wanamkaribisha mgeni kwani atashiriki kwa sana tu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram alisema

"Mchezo umegeuka, nimesaini mkataba wa miaka 10 kutumbuiza katika tamasha la Camp Flog Gnaw, naombeni radhi watoto tutaonana kila mwaka hadi wote mtakapofikisha miaka 30" alimalizia kwa kuweka emoji ya kucheka.

# Khalid ashika namba mbili umaarufu



JARIDA moja nchini Marekani liitwalo Time, limemtaja rapa Khalid kuwa anashika nafasi ya pili kwa umaarufu mwaka 2019.

Mtu aliyeshika namba moja ni mke wa Rais mstaafu nchini Marekani aitwae Michelle Obama, ambao wote wapo katika orodha ya watu kumi ambao ni maarufu nchini Marekani.

Khalid ambaye ana miaka 21 rekodi zake zinaendelea kukubalika duniani kutokana na ladha ya muziki wake.



## Davido unawapa tabu sana

NANI kasema ilikuwa nguvu ya soda? Basi kama huamini kwa mara nyingine mwanamuziki nyota wa Nigeria, Davido, kamzawadia msanii mwenzake Zlatan mkufu wenye thamani ya Sh.milioni 90.

Kama unakumbuka mnamo mwezi Octoba 15, mwaka huu Davido alimpa msanii huyo zawadi ya mkufu wa milion 19.

Davido na Zlatan wameanza maswali yasiyo na majibu nchini Nigeria huku wengine wakisema huenda Davido anafanya maandalizi ya kumsainisha msanii huyo kwenye lebo yake.

## Prezzo atishia nyau wazushi

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Prezzo, ametishia kuwashtaki wale wote waliomzushia eti kabakwa na wanawake watatu hadi kulazwa hospitalini kwa matibabu.

Prezzo alikanusha taarifa hizo na kusema hazina ukweli kwani yeye yupo salama na kwamba hajakutana na kitu kama hicho.

"Sijafanywa chochote na kile kinachosambaa kwenye mitandao hakuna ukweli wowote, mimi nipo salama na wale wote waliosema uongo nitawashtaki," amesema.





## AKA atoa ushauri kwa Burna Boy

RAPA mkali kutoka Afrika Kusini, AKA, amemtaka mwimbaji mwenzake wa Nigeria, Byrna Boy, kuchukua hatua sahihi wakati uhusiano wa nchi hizo umerudi tena.

AKA alisema maneno hayo baada ya kuombwa msamaha na Burna ambaye awali aliapa kutokwenda tena nchini humo kutokana na vurugu zilizokuwa zikiendelea.

Burna hakushiriki katika tamasha la amani lililofanyika Afrika Kusini na kusababisha hali ya wasiwasi kwa mashabiki wa muziki.

## Msimuonee donge Uriel akitumia fedha

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), Uriel, amesema manunuzi aliyofanya akiwa Dubai yanatokana na pesa zake binafsi.

Amesema katika suala la matumizi kwake si jambo geni na kwamba hata mastaa wa nchi hiyo wanatumia pesa walizochuma kwa jasho lao.

Uriel alianza kusema hayo baada ya kuibuka mjadala mkali katika mitandao ya kijamii baada ya picha zake zikimuonesha akinunua bidhaa katika maduka ya kifahali kusambaa kwa kasi.



SAFU



Na John Juma
0716217615

## MIONZI YA SHERIA

# Ni halali kujadiliana na DDP, kufutiwa kesi

ZAMA hizi si tatizo tena kuanza kuwaza kuwa hivi inawezekana au sheria za Tanzania zinaruhusu washukiwa au washitakiwa kujadiliana na Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP) na kufikia makubaliano ya kumaliza kesi nje ya mahakama na hata kesi kufutwa?

Kimsingi, swali hilo limejibiwa na hata kama linaendelea kuwasumbua wachache ni jukumu lao kujua kuwa hakuna kikwazo na yote sasa yanawezekana.

Msingi wa makala hii ni hatua za hivi karibuni zilizofanyika nchini kufuatia ushauri wa serikali kwa washtakiwa wa makosa ya uhujumu uchumi kushauriwa kuomba radhi na kutubu mashtaka yao.

Serikali iliwaagiza wahusika kuandika barua kuamba radhi, kukiri makosa na kukubali kurejesha kiasi cha fedha wanachodaiwa. Kauli au ushauri huo wa Rais, John Magufuli,

Rais aliitoa Jumapili Septemba 22, 2019 akiwa Ikulu jijini Dar es Salaam, akimshauri

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kuwasikiliza mahabusi wanaoshtakiwa kwa kesi za uhujumu uchumi.

Aidha, alitangaza kuwa wale watakaokiri, kuomba radhi na kukubali kurudisha fedha wanazodaiwa wasamehewe na kufutiwa mashtaka.

Alisema katika baadhi ya kauli zake:"Najua wanateseka. Unaona wanavyopelekwa mahakamani, wengine wamekonda kweli. Inatia huruma na inaumiza. Najua wengine wanataka kuomba msamaha...wale ambao watakaoshindwa kuomba msamaha, waendelee kubanwa hata kama kesi zao zitachukua miaka 20."

**MATOKEO**

Baada ya ushauri huo matokeo ya utekelezaji wake yamekwenda kama ambavyo taarifa zimekuwa zikitolewa.

Itakumbukwa kuwa , Septemba 5 mwaka huu Bunge la Tanzania lilipitisha muswada wa maboresho ya sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambapo mapatano baina ya watuhumiwa na Mwendesha Mashtaka (plea bargain) yalipitishwa.

Kwa mabadiliko hayo yeyote kati ya mtuhumiwa, wakili wake ama mwendesha mashtaka anaweza kuanzisha mapatano hayo kwa kuifahamisha mahakama juu ya suala au nia hiyo ya kufanya majadiliano nje ya kizimba.

Kisha kuanzia hapo mahakama kwa upande wake haitahusika tena na makubaliano hayo.

Katika makubaliano hayo , mshukiwa au mshitakiwa anaweza kukiri tuhuma au sehemu ya tuhuma dhidi yake

ili kupata afueni fulani ikiwamo kufutiwa mashitaka au kuondolewa baadhi ya mashtaka na hata kupunguziwa muda wa kutumikia adhabu au aina ya adhabu.

Halikadhakika, anaweza kutakiwa kulipa fidia ama kurejesha fedha ambazo zinahusishwa na kesi

anayoshitakiwa nayo, kama ambavyo Rais alitangulia kushauri.

**MUSWADA**

Ni muhimu kusema kwa mujibu wa muswada huo, makubaliano hayo yakishafikiwa, yatapelekwa au kuwasilishwa mahakamani ili kutambuliwa rasmi, lengo ni mahakama katika hatua ya awali, ijiridhishe kuwa hayakuingiwa kwa shuruti.

Bado, mshukiwa atatakiwa kula kiapo cha kukubaliana na makubaliano hayo, pamoja na mhusika kusomewa haki zake za msingi ikiwamo "kumuondoshea haki ya kukata rufaa" isipokuwa kuhusu kurefusha muda au kipindi au uhalali wa hukumu atakayopatiwa .

**MUHIMU**

Makubaliano hayo kwa mujibu wa muswada hayatafanyika kwa watuhumiwa wa makosa kama udhalilishaji wa kingono ambayo adhabu yake inazidi kifungo cha miaka mitano ama inahusisha walalamikaji wa chini ya miaka 18.

Mengine ni mashtaka ya uhaini, kumiliki ama kusafirisha dawa za kulevya ambazo thamani yake ni zaidi ya Sh. milioni 10, ugaidi, kukutwa na nyara za serikali ambazo thamani yake ni zaidi ya milioni 10 bila kibali maalumu cha maandishi cha DPP.

Isitoshe, ni mshitakiwa pekee ndiye atatakiwa kuiandikia Barua Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashitaka wa Serikali kwa kupitia Mkuu wa Gereza alipo na siyo wakili wake au mtu mwingine yeyote.

Halikadhalika , muswada huo, kwa mujibu wa utaratibu, kama ilivyo kwa miswada mingine, baada ya kupitishwa na Bunge ulisainiwa na rais hivyo wenyewe ni sheria rasmi na halali kuanzia hapo.

Ibara ya 97(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977; kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.



Na Reubeni Lumbagala

## KALAMU YA MWALIMU

# Mkumbuke takwimu sahihi huboresha elimu

TAKWIMU ni njia ya kitaalamu ya kupata taarifa sahihi ili hatua zaidi zichukuliwe. Ndiyo maana kila baada ya miaka 10 hufanyika sensa ambayo inalenga kupata takwimu sahihi za idadi ya watu ili shughuli mbalimbali za kiserikali hasa za kimaendeleo zinapofanyika ziweze kuzingatia mahitaji halisi ya raia wake.

Halikadhalika, katika sekta ya elimu, suala la takwimu lipo na linapewa msisitizo na hii imepelekea hata katika Idara ya Elimu - Msingi na Sekondari kuwapo na Maofisa Elimu Vifaa na Takwimu wanaoshughulikia masuala ya takwimu ili kuchagiza maendeleo ya elimu na taaluma kwa ujumla hasa kwa idadi ya mahitaji halisi.

Mwezi uliopita, Baraza la Mitihani Tanzania (Necta) lilitangaza matokeo ya kuhitimu Elimu ya Msingi ya darasa la saba kwa mwaka 2019, ambapo matokeo yalionyesha ufaulu wa wanafunzi ni asilimia 81.50 sawa na ongezeko la asilimia 3.78 ikilinganishwa na mwaka 2018.

Kutokana na asilimia kubwa ya wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao ya darasa la saba, kundi kubwa linatarajiwa kujiunga na elimu ya sekondari mapema Januari mwaka 2020.

Kwahiyo, shule za sekondari za serikali zitapokea kundi kubwa la wanafunzi mwakani kwa mujibu wa matokeo haya. Maofisa elimu wa wilaya na mikoa wanawajibika moja kwa moja katika zoezi la kuchagua wanafunzi wa kujiunga na shule za sekondari zilizopo katika wilaya na mikoa yao.

Novemba 1, 2019, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Joyce Ndalichako, akiwa katika ziara ya kikazi ya ukaguzi wa ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Kilimo ya Kilosa mkoani Morogoro aliwaonya Maofisa Elimu wa Mikoa wanaoidanganya serikali kuwa wamemaliza tatizo la upungufu wa madarasa.

Waziri Ndalichako alisema maofisa hao wanaongeza idadi ya wanafunzi katika shule za zamani na kusababisha wanafunzi hao kufanya vibaya katika mitihani yao ya kitaifa.

Ni vyema maofisa waliopewa jukumu la kusimamia sekta ya elimu ambayo ndiyo mapigo ya moyo ya taifa letu wakasimamia kikamilifu elimu yetu huku suala ya ubora wa elimu na miundombinu yake likitiliwa mkazo mkubwa. Ndalichako alisema ameamua kuzungumzia suala hili wakati huu ambao maofisa elimu wanakwenda kushiriki kwenye kazi ya kuteua wanafunzi wa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Kila Mkuu wa Shule ya Sekondari anapendekeza idadi ya wanafunzi wa kujiunga na shule anayoiongoza kwa kuzingatia uwepo wa rasilimali madarasa na nguvukazi ambayo ni walimu ili kufundisha na kujifunza kufanyike katika mazingira bora na hatimaye kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa, ujuzi na stadi kutoka kwa walimu wanaofundisha. Hapa ndipo suala la takwimu sahihi linapochukua nafasi yake.

Kwa agizo la Waziri Ndalichako, tunategemea Maofisa Eimu watazingatia takwimu sahihi watakazopewa na wakuu wa shule ili shule zipokee idadi ya wanafunzi watakaoweza kuhudumiwa kikamilifu.

Aidha, Maofisa Elimu warejee agizo la Waziri Ndalichako la kusema ukweli mara wanapotoa ripoti za hali ya miundombinu ya elimu katika shule zao. Hakuna sababu ya maofisa elimu kutoa takwimu za uongo kwa kudhani kwa kufanya hivyo wanamfurahisha Rais John Magufuli, huku wakichangia kushusha ubora wa elimu kwa kurundika wanafunzi wengi darasani na kuwaongezea walimu ugumu wa kazi ya ufundishaji.

Wingi wa wanafunzi hao unawapa walimu ugumu wa kiutendaji kutokana na kuhudumia wanafunzi wengi kuzidi uwezo alionao.

Ni heri, tatizo la upungufu wa madarasa, madawati, vyoo, walimu likaonekana ili serikali iweze kulishughulikia kuliko kuficha changamoto hiyo kwani mficha maradhi, kifo humuumbua. Ikumbukwe kuwa serikali yetu imeamua kwa vitendo kugharamia na kufadhili miradi mbalimbali ya elimu ili kuweza kuboresha sekta ya elimu. Mathalani, kila mwezi, Sh. bilioni 24 zinatumika kugharamia sera ya elimu bila malipo.

Kwa awamu saba za utekelezaji wa mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R), Sh. bilioni 306 zimeshatumika katika uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari nchi nzima. Kwa awamu ya nane ya Mradi wa EP4R, Sh. bilioni 201 zimeshatengwa kwa ajili ya kuboresha na kujenga miundombinu ya shule nchini.

Haya yote ni kielelezo tosha kuwa serikali inao uwezo wa kushughulikia changamoto za miundombinu ya shule zetu pindi takwimu sahihi zitakapoifikia serikali.

Utoaji wa takwimu sahihi utasaidia maendeleo ya elimu yetu kwani uhitaji utakapoonekana, serikali itachukua hatua stahiki za kutatua changamoto hizo.

Ni vyema maandalizi ya kuboresha na ujenzi wa miundombinu ya shule yafanyike sasa ili wanafunzi watakaojiunga kidato cha kwanza na wale wa darasa la kwanza mwakani wakute mazingira mazuri ya kujifunza bila kupoteza muda wa kusubiri ujenzi wa miundombinu ukamilike, ndipo waanze masomo. Tutafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma.
**Maoni: 0764 666349.**

MAKALA

# Kilimohai kinavyoigeuza dunia Bustani ya Edeni

**Na Faustine Feliciane**

DUNIA kwa sasa inashuhudia mabadiliko ya tabianchi huku juhudi kubwa zikifanywa katika kuyamudu na kuendeleza maisha.

Changamoto ya mabadiliko ya tabianchi inawapa wanasayansi na wanadamu jukumu la kutafuta majawabu ili kuifanya dunia kuendelea kuwahifadhi watu, wanyama na viumbe wengine.

Mojawapo ya maeneo ambayo wanasayansi wanayahangaikia ni kufanikisha upatikanaji wa mbegu za mazao mbalimbali zinazoweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi ili kuendeleza kilimo na kuwa na uhakika wa chakula.

Mengi yanajadiliwa juu ya suala la mbegu, lakini pia juu ya nini kimeifikisha dunia hapo ilipofikia.

Ikumbukwe kwamba mabadiliko ya tabianchi si jambo la nadharia tena, bali ni suala ambalo lipo katika maisha ya kila mtu, hivyo ni lazima kupambana nalo kwa nguvu na maarifa.

Wakati wanasayansi na kampuni kubwa zikiwekeza fedha nyingi kwenye utafiti wa mbegu zikiwamo zilizobadilishwa vinasaba kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, wengi hawajarudi na kujitafakari dunia imefikaje hapa na ni ipi njia sahihi ya kuinusuru kutokana na uharibifu uliotokana na kazi za binadamu.

Hofu ya mabadiliko ya tabianchi imesambaa si tu kwa wanasayansi, bali wanasiasa na sasa hata kwa wakulima ambao kwa namna moja au nyingine athari hizi zimeanza kuwakumba.

Miongoni mwa athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi zinazoathiri shughuli za uzalishaji katika kilimo mashambani ni pamoja na kuwapo kwa magonjwa mengi kwa mazao yalimwayo kwa sababu ya ama ukame au mvua kunyesha kupita kiasi au kwa viwango pungufu kama ilivyozoeleka na wakulima wengi.

Changamoto nyingi zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa sehemu kubwa suluhu yake ni uhifadhi wa mazingira lakini pia upunguzwaji wa hewa ukaa kwa mustakabali wa maisha endelevu.

Hivi karibuni, Shirika la Kuendeleza Kilimo Hai Tanzania (TOAM), kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) yamejitokeza hadhara kwa kuwajengea uwezo na maarifa waandishi wa habari ili waweze kuwa na uelewa mpana wa kuandika na kukitangaza kilimohai.

Jukumu la msingi ni kuhakikisha sekta ya kilimohai inaendelezwa na kupanuka ili kujibu malengo endelevu kama inavyopambanuliwa katika maeneo zaidi ya manne ya malengo endelevu.



Kilimo hai huchanganya mazao mengi kwenye eneo moja, mathalani kahawa na ndizi zimepandwa pamoja. Mimea hiyo ni muhimu kwani hurutubisha ardhi pia hutumia hewa ukaa na kupunguza joto duniani. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE.**

Mshauri wa mawasiliano wa shirika hilo Constantine Akitanda, anaelezea jinsi kilimohai kilivyobeba siri kubwa ya maisha ya mwanadamu, kuanzia uchumi, afya, mazingira na hata kuyakabili mabadiliko ya tabianchi.

Kuhusu uendelevu katika kilimo, Akitanda anafafanua kuwa mabadiliko kadhaa yanayojitokeza katika mazingira ya sasa u si jambo lililotokea usiku mmoja, bali ni matokeo ya siku nyingi yaliyosababishwa na kilimo na kazi za uzalishaji zisizozingatia uhifadhi.

Anasema jukumu la sasa ni kuendesha kilimo kwa njia zilizoendelevu wakati huo pia wa kuweka uwiano sawa wa kiikolojia ili kuendelea kulinda rutuba ya udongo na kuepusha wadudu wavamizi.

Ofisa huyu wa mawasiliano, vilevile anasema kilimohai kinapingana sana na dhana ya kukiri tatizo baada ya kutokea, badala yake kilimohai chenyewe kinajielekeza zaidi katika kulinda mifumo ili kujiepusha na athari zaidi kwa kuwa mifumo yenyewe ina utaratibu wa kujilinda usipoivuruga.

Kuhusu kuurutubisha udongo chini ya mfumo huu wa kilimohai Akitanda, anaeleza kuwa kuna utamaduni au utaratibu uliothibitishwa kitaalamu ambao ni lazima kizingatie mzunguko wa mazao katika shamba.

Aidha, vile vile mkulima wa kilimohai ananyongeza ya maarifa ya kuhakikisha udongo unalindwa hata kwa kuwekewa matandazo ili kuzuia miale ya jua kunyonya akiba ya maji iliyopo kwenye ardhi na kuuondolea udongo uhai kwa kuviumiza au kuviua viumbe hai kwenye ardhi.

Mkulima wa kilimohai pia atawajibika kubakisha shambani mabaki yote ya mabua au majani baada ya kumaliza kuvuna, mabaki hayo huozea shambani na kuliongezea shamba uhai na rutuba. Akitanda, anasisitiza kuwa katika mazingira ya kulilinda na kuliboresha shamba, mkulima haruhusiwi kuchoma moto shamba lake baada ya mavuno.

"Hii ni mojawapo ya siri kubwa katika uhifadhi wa mazingira lakini ni muhimu katika kuliimarisha shamba na kuliongezea uhai sambamba na rutuba." Anasema Akitanda.

Anahimiza pia kulima mazao mchanganyiko katika shamba moja, matumizi ya mbolea hai isiyo ya kemikali pamoja na ukulima wa kutoufukuza sana udongo kuwa ni miongoni mwa njia zinazohimizwa sana unapoamua kufuata mfumo huu.

Katika maelezo yake, Akitanda anasema kuwa, mfumo wa kilimohai ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha uhifadhi wa maji kwenye eneo linalolimwa, kuchafuka kwa maji chini ya ardhi kunakofanywa na kilimo kinachotumika kemikali pamoja na sumu zinazopulizwa mashambani kuua wadudu ni janga linalotafuna dunia sasa na hata siku zijazo.

Ingawa uharibifu wa mazingira siyo jambo linalofanywa siku moja, bali ni mchakato unaofanyika na kufikia kiwango cha juu baada ya muda mrefu hadi madhara yanapotokea.

Hoja hii ya uharibifu inaungwa mkono na Ofisa Mawasiliano wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Emmanuel Kihaule , ambaye pia ni mwandishi wa masuala ya mazingira.

Kihaule anasema, ni jukumu la kila mmoja kujihusisha na suala zima la uhifadhi wa mazingira ili kuleta uendelevu wa maisha ya mwanadamu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

"Kila mmoja anayo haki ya kuchagua mfumo wa kilimo, lakini kilimohai kwangu ni endelevu na chenye tija kwa vizazi vingi.Tukikitumia kitatulinda na kutuvusha tukiwa salama, hiki pia kinatusaidia kulinda maji yetu yabaki yakiwa salama."

Kuhusiana na hewa ukaa na mabadiliko ya tabianchi, kilimohai, kinatajwa kutoa mchango mkubwa katika kupunguza uhitaji wa matumizi ya mbolea za kemikali katika shamba pamoja na nishati rejelevu kwa kuwa nishati hizi zinahitaji malighafi nyingi kuzizalisha na hivyo kuathiri mazingira na kuchangia mabadiliko ya tabianchi.

Katika hali kama hiyo, kilimohai ndicho kinachoonekana kusaidia kukabiliana na madhara ya hewa ukaa na kudhibiti ongezeko la joto duniani kwa kuwa kina uwezo wa kuitumia hewa hiyo iliyoko ardhini, pasipo kuleta madhara kwenye hewa.

Njia karibu zote zinazofuatwa na mfumo wa kilimohai katika ukulima ikiwamo mzunguko wa mazao, ukulima wa mikunde kwa lengo la kuongeza naitrojen ardhini, mchanganyiko wa mazao, kufukia mabaki ya mazao ardhini kwa kiwango kikubwa kunasaidia kuikabali hewa ukaa kubakia ardhini na hivyo athari zake kutoifikia dunia na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Kihaule anasema utafiti umebainisha kuwa uzalishaji mazao chini ya mfumo wa kilimohai husaidia kudhibiti hewa ukaa iliyoko ardhini, nchi zinazoendelea karibu zote hazijaweza kuweka mifumo taarifa kuhusu kiwango cha hewa ukaa katika udongo kwenye mashamba yanayolimwa jambo alilosema ni muhimu kuanza kutekelezwa.

**MAKALA**

# Mguu kifundo unatibiwa usimfiche mtoto mlemavu

**Na Mwandishi Wetu**

KILA mwaka zaidi ya watoto 100,000 duniani huzaliwa na ugonjwa wa mguu kifundo 'Clubfoot' ambacho humkwamisha mtoto kutembea kwa kutumia unyayo na badala yake hukanyagia kifundo cha mguu.

Taarifa hii si nzuri masikioni mwa Salma Hajj (29) mkazi wa Buza Jijini Dar es Salaam, ambaye miezi 10 iliyopita alijifungua mtoto akiwa na tatizo hilo ambalo kisayansi linaelezwa kuwa linatokea hata kabla mtoto kuzaliwa.

"Ilikuwa ni furaha moyoni mwangu kwani nilitegemea kupata mtoto, tena akiwa mwenye afya njema, lakini furaha yangu ikageuka kuwa huzuni baada ya kujifungua kwani sijui ni jambo gani limemsibu hata akazaliwa na miguu iliyojikunja," anasema Salma

Kwa Tanzania, inakadiriwa kuwa karibu watoto 2,800 wanazaliwa na ugonjwa kama wa mtoto wa Salma, wakati huo, kati asilimia 50 wana athirika mguu mmoja huku waliobaki wakiathiriwa miguu yote miwili, kwa mujibu wa Hospitali ya CCBRT ya jijini Dar es Salaam.

**ATHARI**

Hospitali hiyo ya CCBRT inasema kuwa asilimia 80 ya wagonjwa wasiopata matibabu mapema wanapatikana kwenye nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania.

Na kwamba ugonjwa huo usipotibika unaweza kusababisha maumivu makali wakati wa kutembea na hatimaye husababisha ulemavu.

"Kiukweli ulikuwa ni wakati mgumu sana kwangu.Nilijisikia vibaya kwamba mwanangu hataweza kutembea vizuri. Hata hivyo, sikujua anasumbuliwa na tatizo gani kwa kipindi kile.," anasema Salma.

AIdha, anaongeza kuwa:"Nilihisi kama ilikuwa mwisho wa dunia kwangu na mwanangu, nilijiuliza maswali mengi bila majibu kwamba atawezaje kutembea? Ataonekanaje kwa watu? Atasoma katika shule gani? Nilichanganyikiwa sana," anasema mama huyu.

Baada ya kupewa taarifa kuwa katika hospitali ya CCBRT wanatibu ugonjwa uliomkuta mtoto wake alifanya jitihada za kumpeleka kwa ajili ya kuonana na wataalamu.

**TIBA**

Salma anasema, "kuna kipindi alikuwa anapitia wakati mgumu kwani alikuwa analia sana jambo lililonifanya na mimi kulia. Nilikuwa na wasiwasi juu ya maisha ya mwanangu siku za mbeleni," na kuongeza kuwa;

"Nawashukuru sana kampuni ya Tigo na madaktari wa CCBRT kwa msaada wao mkubwa kwa sababu sasa hivi mwanangu ana miezi 10 na amepona kabisa."



Madaktari wakirekebisha mguu wenye kifundo. **PICHA: TIGO**

Mwezi uliopita kampuni ya Tigo ilirudisha tabasamu na matumiani kwa wazazi na watoto wanaosumbuliwa na ugonjwa huo kwa kutoa msaada wa Sh.milioni 100 kwa ajili ya kusaidia matibabu kwa watoto wenye ugonjwa huo waliopo hospitalini na wale wa majumbani.

Ofisa wa Uwajibikaji kwa Jamii wa Tigo, Halima Okash, anasema kampuni hiyo imeona umuhimu wa kuwasaidia watoto wenye ugonjwa huo ili kutimiza ndoto zao na kuleta furaha kwa wazazi wao.

**1,509 WANUFAIKA**

Ofisa Okash, anasema kuwa kupitia msaada huo kutoka Tigo, CCBRT inaweza kutoa huduma za matibabu kwa njia 'ponseti' bila upasuaji kwa wagonjwa wapya zaidi ya 400 na wengine wanaoendelea na matibabu hospitalini hapo.

"Tuliona kuna umuhimu wa kusaidia wahitaji hawa kwasabau CCBRT inahudumia jamii yenye uhitaji na wasiojiweza katika kuwasaidia kupata huduma za matibabu.Tumeunga mkono jitihada hizi zinazofanywa na hospitali hii kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata nafasi ya kutibiwa kwa gharama ndogo au bure kabisa," anasema Okash.

Vilevile, anaeleza kuwa kupitia huduma za upasuaji kutoka CCBRT jumla ya watoto 1,509 wamenufaika kwa kipindi cha miaka sita iliyopita.

"Haya ni mafanikio yanayotufanya Tigo kujisikia faraja kwa kiasi kikubwa kwani kwa kutoa matibabu kwa watu wanaoishi na ulemavu kwa pamoja tunaleta matokeo chanya kwa maisha ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii ya Tanzania yote," anasema Okash.

**TIBA YA MIDOMO**

Okash anaongeza kuwa tangu mwaka 2013, Tigo iliingia ubia na hospitali ya CCBRT kutoa matibabu kwa wagonjwa wa midomo sungura, kwa kutumia njia ya ujumbe mfupi -SMS zinazotumwa kwa wagonjwa wa CCBRT kuwakumbusha kufuatilia matibabu na kutoa uelewa kuhusu huduma kwa umma.

Anasema kupitia mpango huu, wagonjwa wanaweza kupata ujumbe wa matibabu kwa siku nne na siku moja kabla ya siku ya matibabu na hii imeisaidia CCBRT kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokatisha matibabu.

"Kupitia mchango huu tunaendelea kudhihirisha dhamira yetu ya kusaidia kujenga taifa la watu wenye afya ambao wataweza kuchangia katika shughuli za kimaendeleo na pia nitoe wito kwa wadau wengine kuungana na CCBRT ili kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii yetu," anasema Okash na kuongeza;

"Tigo imeonyesha mfano wa kazi ya sekta binafsi katika kutoa suluhisho kwa matatizo yanayozikumba jamii zetu. Kwa miaka kadhaa CCBRT imefanikiwa kutatua changamoto ya matibabu ya ugonjwa huu wa miguu kifundo kwa kuhakikisha wagonjwa wanapatiwa huduma endelevu pamoja na ufuatiliaji wa mara kwa mara," anasema.

**CHANZO KIFUNDO**

Kwa mujibu wa daktari wa mifupa (Orthopedic) wa CCBRT, Dk. Zainab Ilonga, chanzo cha ugonjwa huo bado hakijulikani.

Anasema hadi sasa sababu yake bado haijathibitika, lakini, wataalamu wanaamini kuwa moja ya sababu ni matumizi ya pombe na matumizi mabaya ya madawa wakati wa ujauzito au urithi wa vinasaba (genetic) na kubainisha kuwa tafiti zaidi zikifanywa zitasaidia kutambua chanzo halisi cha tatizo hilo.

"Kuna njia mbili za kutibu ugonjwa huu wa mguu kifundo; moja ni kutumia ponseti ambayo haihitaji kufanya upasuaji na nyingine ya kufanya upasuaji.," anasema Dk Ilonga.

Aidha, anaongeza kuwa kwa Tanzania wanatibu watoto takribani 400 kwa mwaka sawa na asilimia 25 ya wagonjwa wote na hiyo inatokana na baadhi ya wazazi kuwaficha watoto wenye tatizo hili. Anaeleza kuwa 'Ignacio V. Ponseti' ni njia ambayo imekuwa ikitumia kutibu mguu kifundo tangu miaka ya 1940, na moja ya kanuni zake ni kwamba tishu za mtoto ikiwamo 'tendoni' misuli inayounga mfupa na mfupa mfano goti na ligament ambayo ni misuli inayounga mfupa na mfupa na maungio yake yapo katika hatua za mwanzo za ukuaji hivyo kufanya mguu kuungana baada ya kila wiki moja.

Anafafanua kuwa kwa kutumia njia hiyo ndani ya wiki kadhaa hali ya mgonjwa inaweza kubadilika na kufanikisha kuurekebisha mguu bila uhitaji wa kufanya upasuaji.

"Mtoto wa Salma alipitia hatua hiyo maarufu kama 'gentle bone manipulations' na ufuatiliaji (castings) ili kujua mabadiliko ya kibaiolojia hasa misuli yake, maungio na tishu kwa lengo la kutibu tatizo alilokuwa nalo," anasema.

Anawahimiza wazazi na walezi kuacha kuwaficha watoto wenye tatizo hili na kuwafikisha hospitalini kwa matibabu haraka iwezekanavyo.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 20 00)



**Dondoo: Kulia**

2. Bei ya kitu
9. Acha mdomo wazi
10.Hongo
11.Eneo lenye hali fulani ya hewa 13.Wengu
15. Mmea mkubwa
16. Anayejua zaidi 17. Kijiji
18.Ndege aletaye msiba
19.Valleta ni mji wake mkuu
20.Mjumbe wa Mungu
21.kipaji 23.ujenzi wa kutumia mawe 25. kitoweo
27.Badilisha kwa fedha
28.Tia makali kisu
29.Hutumika kupima uwezo wa Mwanafunzi

**Dondoo: Chini**

1. Kichwa
2. Ghuba ya Uajemi
3. Faini
4. Tunu
5. Hutumika kurandia mbao
6. Punje za mtama
7. Bei ya kitu
8. Eleweka
12.Ishara
14. Fuatana
17.Ndege mweusi baka jeupe
19. Wingi wa neno msingi
22.Utulivu uliopo mahali
24. Mmea wa nyasi
26. maoni

## Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Z | A | N | Z | I | B | A | R | | B | | | C |
| A | | U | | | | G | | S | A | R | A | H |
| M | A | K | U | M | B | U | S | H | O | | | E |
| A | | U | | A | W | A | L | I | | | | K |
| N | Y | U | M | B | A | | A | A | L | I | | E |
| I | | | K | A | N | S | A | | | | | C |
| | M | K | O | B | A | | | A | B | A | | H |
| K | A | I | M | U | | M | N | Y | O | N | G | E |
| | U | S | A | | G | I | D | A | M | U | | A |
| M | D | U | N | D | I | K | O | | B | | K | |
| | H | | Z | | T | A | A | R | A | B | U | |
| F | U | N | I | K | A | | N | | | | S | |
| | I | | | | A | D | A | B | I | S | H | A |

# ‘Ndivyo kilometa 100 za lami zinavyoifanya Musoma pepo’

**Na Sabato Kasika**

NI sehemu yenye madini hasa dhahabu, mabonde ya kilimo na ufugaji, lakini pia ni makazi ya aina zaidi ya 200 ya samaki wanaouvuliwa ndani ya Ziwa Victoria, la tatu kwa ukubwa duniani likiwa na maji mengi na ya kutosha matamu na ya baridi.

Mahali hapa ni Wilaya ya Musoma na hasa upande wa jimbo la Musoma Vijijini ambalo linatajwa kuwa na fursa nyingi za kiuchumi na kijamii, kwa vile lina sifa zote za kiuchumi zinazofanikisha na kuurahisisha uwekezaji kutokana na upatikanaji wa rasilimali na maliasili zote muhimu kwa ajili ya shughuli zote za kiuchumi.

Hata hivyo penye uzuri hapakosi kasoro, ukosefu wa barabara zenye kiwango cha lami kwa miongo mingi ni miongoni mwa matatizo yanayotajwa kuchangia kukwamisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanayoibuliwa na fursa za kiuchumi zilizoipamba Musoma Vijijini.

Lakini yaliyopita si ndwele, shida hiyo inakoma na matatizo hayo yanaisha, kufuatia kuanza kwa ujenzi wa barabara kuu ya kutoka mjini Musoma hadi Busekera ambayo ina urefu wa kilometa 92, ikiunganisha vijiji mbalimbali vya Musoma Vijijini.

Ujenzi wa barabara hiyo ulioanza miezi miwili iliyopita na unatarajiwa kukamilishwa mwaka 2021, hatua ambayo inaelezwa na Mkuu wa Wilaya Musoma, Dk. Vincent Anney, kuwa itaimarisha fursa nyingi za kiuchumi.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Dk. Anney anasema, siyo kuimarisha tu bali zitaibuka fursa nyingine mpya za kiuchumi, kwa vile zipo nyingi, ambazo hazijaibuliwa.

“Ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ulianza miezi miwili iliyopita kwa kilometa tano za awali kuanzia kijiji cha Kusenyi hadi kitongoji cha Kwikonera ndani ya kijiji cha Suguti,” Dk. Anney anasema.

Anaeleza kuwa , mkandarasi akimaliza eneo hilo, ataanzia Kwikonero hadi Busekera na kisha atarudi Kusenyi kuendelea na ujenzi hadi mjini Musoma, ili kumalizia kilometa zote 92 za barabara hiyo.

“Hizo kilometa tano zinazojengwa sasa zitachukua muda wa miezi sita na mkandarasi ameanzia eneo hilo kwa kuzingatia hospitali ya wilaya inajengwa katika kitongoji cha Kwikonero, kijiji cha Suguti,” anasema.

FURSA ZA KIUCHUMI

Mkuu wa Wilaya anasema, Musoma Vijijini ina fursa nyingi za kiuchumi ambazo anaamini ujenzi wa babarabara hiyo kwa kiwango cha lami utachangia kuziboresha na pia zitaibuliwa nyingine mpya.



Mkuu wa Wilaya Musoma, Dk. Vincent Anney, akimwaga mafuta ya taa kuteketeza nyavu haramu eneo la Bwai Kumsoma. **PICHA: SABATO KASIKA.**

Anataja madini akisema;” kwa upande wa migodi ya dhahabu ipo kadhaa kwenye vijiji vya Chirorwe, Ukungu na Seka huko kuna kampuni ya MMG inayochimba dhahabu kijijini Seka,” anasema Anney.

Vile vile anasema kuwa kuna mgodi wa Nyarufu uliopo kijiji cha Murangi na mingine mingi, na kwamba yote hiyo ina fursa za kiuchumi kwa Musoma Vijijini na pia anataja kuwapo viwanda viwili vya kuchakata mafuta ya alizeti ambavyo viko katika vijiji vya Kusenyi na Saragana, pia kuna vya kuchambua pamba vya pamba na kuna mabonde ya kilimo na ufugaji huko Suguti na Bugwema.

“Mabonde hayo yanafaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali yakiwamo ya biashara, hivyo kuwapo kwa lami kutarahisisha usafirishaji wa mazao kwenda katika masoko ya ndani ya nje ya Musoma Vijijini,” anasema.

Aidha, anasema, ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami unakwenda sambamba na maandalizi ya eneo hilo kuwa wilaya, hivyo kuna mkakati wa kuanzisha viwanda mbalimbali vikiwamo vya kuchakata dagaa.

“Siyo hapo tu bali tunatarajia pia kuwa na viwanda vya chakula cha kuku na fish cage farming, na tutaendelea kuboresha shughuli mbalimbali za kiuchumi kadri inavyowezekana, kwa sababu fursa zipo,” anasema Anney.

WANANCHI WAFURAHIA

Kuwapo kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kumewapa matumani mapya baadhi ya wakazi wa vijiji vya Kusenyi na Suguti, ambao wanaamini kwamba sasa wataepuka adha ya kukwama barabarani mvua zinaponyesha.

Sadick Chiguma wa kijiji cha Suguti ni miongoni mwao, ambaye anasema eneo hilo lina udongo mwekundu na tena wa kunata, ambao wakati wa mvua umekuwa ukisababisha magari kukwama.

“Lakini sasa ninaamini kwamba suluhisho la kudumu limepatikana kufuatia mkandaraasi kuanza kwenye eneo hili korofi, hivyo hii ni nafasi yetu kupata lami kwa mara ya kwanza tangu nchi hii ipate uhuru,” anasema Chiguma.

Aidha, kuwapo kwa lami kwenye eneo hilo ni hatua mojawapo ya maendeleo, na anaombea ujenzi wa barabara yote kwa kiwango cha lami ukamilike kwa wakati ili kuboresha huduma za usafiri.

“Umeme tunao na sasa tunaletewa lami, hii ni habari njema kwetu kwani umeme na lami ni mojawapo ya maendeleo, hivyo wananchi hatuna budi kutunza miundombinu ya barabara na umeme,” anasema.

Kwa upande wake Berna Matekere anasema, hiyo ndiyo barabara kuu inayounganisha eneo lote la Musoma Vijijini na kwamba wakulima na wafanyabiashara wanaitegemea.

“Awe mkulima, mfanyabiashara au mtu mwingine yeyote wa huku kwetu, anaitegemea sana barabara hiyo, hivyo uamuzi wa serikali wa kuijenga kwa kiwango cha lami ni wa muhimu kwetu,” anasema Berna.

UFUNGUO WA MAENDELEO

Profesa Sospeter Muhongo ni mbunge wa Musoma Vijijini, anasema, ujenzi huo unaonyesha jinsi maendeleo yanavyoletwa kwa vitendo na kwamba barabara hiyo itawawezesha wananchi kufanya biashara zao kwa uhakika.

“Sasa watafanya biashara kwa uhakika, kwa sababu watafika kwenye masoko kwa wakati na kufanya shughuli zao, na hatua hiyo itasaidia kuwawezesha kuondokana na umaskini,” Prof. Muhongo anasema.

Anasema, serikali imeanza kukata kiu ya wananchi ya kupata barabara ya lami ili kuhakikisha eneo hilo linasonga mbele kiuchumi na kimaendeleo na siyo maneno bila mipango madhubuti.

“Ninashukuru ziara ya waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alioifanya mwaka jana jimboni mwetu kwani ilitusaidia kufikisha ujumbe kwa serikali, hasa kuhusu barabara kuu inayounganisha Musoma Vijijini na mjini,” anasema.

Anasema, barabara hiyo ambayo ni maarufu kama barabara ya Musoma hadi Busekera ina umuhimu mkubwa kiuchumi kwa wakazi wa Musoma Vijijini na kwamba wanafurahia wanapoona inajengwa kwa kiwango cha lami.

“Mimi kama mwakilishi wa wananchi ninajisikia vizuri sana ninapoona serikali ikitujengea barabara kuu kwa kiwango cha lami, ili kurahisisha usafiri na shughuli nyingine za maendeleo,” anasema Muhongo.

# Kenya, Somalia sasa ni shwari

**NAIROBI, Kenya**

KENYA na Somalia, zimekubaliana kurejesha ushirikiano wa awali wa kidiplomasia na kuruhusu raia wa nchi hizo jirani kuvuka mpaka bila vikwazo. Hatua hiyo inakuja, baada ya mazungumzo kati ya Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya na Mohamed Abdullahi Farmajo wa Sudan.

Uhusiano kati ya Mogadishu na Nairobi katika miezi kadhaa iliyopita, ulikuwa kuwa baridi baada ya Somalia kuishtaki Kenya katika Mahakama ya Kimataifa kuhusu mzozo wa mpaka wa bahari kunakopatikana hifadhi ya mafuta.

Katika mkutano wao na waandishi na habari marais hao wawili walionyesha mshikamano kwa kuwaambia waandishi wa habari kwamba Kenya na Somalia ni nchi jirani na ndugu na kubaini kwamba mataifa hayo yameamua kuweka kando tofauti zao na kurejesha uhusiano wao wa awali.

Baada ya mazungumzo yaliyodumu kwa saa kadhaa, Uhuru Kenyatta na Mohamed Abdullahi Farmajo kwanza walionyesha mshikamano wao na kupeana mikono ishara kwamba nchi hizi ni rafiki na ndugu.

Lakini pia, katika taarifa zao kwa wanahabari, wote hawakuweka wazi tofauti zinazokumba na nchi hizi mbili, wakati mikwaruzano baina yao inahusu masuala mengi.

"Hii ni kama ishara ya nia njema, Wakenya na Wasomali watapewa visa wanapowasili nchi mojawapo kati ya hizo mbili, na safari za ndege za moja kwa moja kati ya Mogadishu na Nairobi zitaanza ndani ya kipindi cha wiki moja," alisema Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta.

Kwa upande wa mzozo wa baharini ambao utaamuliwa mwaka ujao na Mahakama ya Kimataifa ya Haki, marais hao hawakuzungumzia lolote. Farmajo ameikaribisha Kenya kwa ushiriki wake katika kikosi cha Umoja wa Afrika AMISOM, na kwa ukarimu wa Kenya kwa wakimbizi wa Kisomali.

Na kusema, "Nina imani kwamba mzozo huu utatatuliwa kwa njia inayokubaliwa ambayo haitaathiri uhusiano wa nchi hizi mbili," akipendekeza mazungumzo ya moja kwa moja.

***Redio Ufaransa***



Mafuriko yaliyotikisa Sudan Kusini na kusababisha mamia kukosa makazi. **PICHA: REUTERS.**

# Israel yatamba kuilipua Gaza

**KHAN YOUNIS, Ukanda wa Gaza**

ISRAEL imetamba kuwa imekamilisha mfululizo wa mashambulizi ya angani katika maeneo yanayohusishwa na kundi la wanamgambo la Islamic Jihad katika Ukanda wa Gaza.

Taarifa ya Jeshi la Israel iliyotolewa mapema jana ilisema inaashiria kuwa nchi hiyo iko tayari kuheshimu mpango wa kusitisha mapigano kama hakutakuwa na mashambulizi zaidi ya makombora.

Jeshi la Israel lilisema limelishambulia eneo moja la kijeshi, kiwanda cha kutengeneza makombora na makao makuu ya wanamgambo katika mji wa Khan Younis.

Hali tete ya utulivu imeshuhudiwa jana nchini Israel na katika Ukanda wa Gaza, baada ya mpango wa kusitisha mapigano uliosimamiwa na Misri kati ya Israel na wanamgambo wa Islamic Jihad kuanza kutekelezwa katika saa za asubuhi. Kwa mujibu wa Jeshi la Israel, hata hivyo, makombora yalifyatuliwa kuelekea Israel kutokea eneo hilo la pwani baada makubaliano hayo kuanza kutekelezwa.

Mos'ab al-Breim, Msemaji wa Islamic Jihad, aliesema kundi lake limedhamiria kuheshimu mpango uliofikiwa na Misri na kwamba kuna makubaliano ya Wapalestina ya kudumisha utulivu uliopo kwa sasa.

Kwa mujibu wa msemaji huyo, makubaliano hayo ni pamoja na kusitishwa kwa mauaji yanayowalenga viongozi wa wanamgambo, kuwalinda waandamanaji wa Kipalestina katika Ukanda wa Gaza na hatua za kuumaliza kuizingira Gaza.

Nickolay Mladenov, Mratibu Maalum wa Umoja wa Mataifa kwa mchakato huo wa Mashariki ya Kati, ambaye alikuwa amekwenda Cairo kusaidia kufikiwa makubaliano ya kusitisha mapigano, aliandika kwenye Twitter ujumbe wa kuzitaka pande zote "kuonyesha kiwango kikubwa cha kujizuia".

Usitishwaji huo wa mapigano haukuthibitishwa rasmi na serikali ya Israel. Lakini msemaji wa Jeshi Jonathan Conricus alisema walifahamishwa kuhusu makubaliano hayo.

Jeshi la Israel juzi Alhamisi liliondoa vizuizi vya usalama dhidi ya jamii zilizoko karibu na Gaza baada ya kuitathmini hali ya sasa. Zaidi ya makombora 450 yamevurumishwa katika maeneo ya kusini mwa Israel tangu Jumanne, kwa mujibu wa jeshi la Israel, huku mengi yakiharibiwa na mfumo wa ulinzi wa angani wa Iron Dome.

Mashambulizi hayo kati ya Israel na wanamgambo wa Kipalestina yamewauwa watu 34 katika Ukanda wa Gaza wakiwamo raia 16, tangu yalipoanza Jumanne kama jibu la mauaji ya Israel yaliyowalenga viongozi wawili wa Islamic Jihad, ambapo moja lilimuua kiongozi wa Quds Brigades Rasmi Abu Malhous, ambalo ni tawi la wapiganaji la Islamic Jihad katika Ukanda wa Gaza.

***DW***

## Mvua ya mafuriko yaathiri 420,000

**JUBA, Sudan Kusini**

TAKRIBANI watu 420,000 wapoteza mali na hawana makazi kufuatia mafuriko makubwa yaliyoikumba Sudan Kusini.

Shirika la kimataifa la misaada la Save the Children limesema zaidi ya watu 420,000 wamelazimika kuondoka kwenye makazi yao kutokana na mvua kubwa zilizosababisha mafuriko nchini Sudan Kusini.

Halikadhalika shirika hilo lilisema, kiasi cha asilimia 60 ya walioondoka, tayari walikuwa wanakabiliwa na utapiamlo mkali, kabla ya kuanza kwa mvua hizo kubwa.

Lilikadiria kuwa kwa ujumla, watu 900,000 ama asilimia saba ya idadi ya jumla ya watu nchini humo wameathirika na mafuriko, hii ikiwa ni kwa mujibu wa shirika hilo la Save the Children.

Aidha shirika hilo limeongeza kuwa ilikuwa ni vigumu kupeleka misaada ya uokoaji kwa watu hao kutokana na mafuriko, hali iliyowalazimu kusitisha upelekaji wa misaada kwenye baadhi ya maeneo na kusababisha hali kuwa mbaya zaidi.

Mkurugenzi wa Save the Children nchini Sudan Kusini, Rama Hansraj, alisema mafuriko nchini humo yamefikia katika kiwango cha kutia wasiwasi na watoto pamoja na familia zao wanahitaji msaada wa dharura, katika wakati huu ambao nchi hiyo inatarajia kunyesha mvua nyingi zaidi wiki zijazo.

**DW**

## BRICS yasisitiza umuhimu wa mageuzi ya kibiashara

**BRASILIA, Brazil**

KUNDI la mataifa matano yanayoinukia la BRICS limesema linaunga mkono ushirikiano wa pamoja wa mataifa duniani unaohusisha biashara huria lakini limekosoa sera za ulinzi wa masoko.

Katika taarifa ya pamoja iliyotolewa wakati wa kufungwa mkutano wa siku mbili uliofanyika mjini Brasilia, nchini Brazil, viongozi wa kundi la BRICS wamesititiza umuhimu wa kuwa na biashara huru ya kimataifa inayozingatia kanuni, uwazi, uhuru na isiyobagua.

Mataifa ya kundi la BRICS ya China, India, Afrika Kusini, Brazil na Urusi yalisema kuwa yanatambua pia umuhimu wa kufanyika mageuzi katika shirika la biashara duniani WTO ili kulipatia nguvu ya kushughulikia changamoto zilizopo na za siku za usoni.

Kadhalika kundi hilo limezungumzia ulazima wa kuimarisha na kufanya mageuzi kwenye mifumo ya kimataifa ikiwamo Shirika la Fedha Duniani (IMF) na mashirika mengine ya kimataifa.

**DW**

# HADITHI

# Jumba Jekundu-27

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

Na Adam Fungamwango (0716 350534)

Kilikuwa ni chumba kikubwa chenye kila kitu kinachopatikana kwenye hoteli za kisasa.

Alijituma kwenye sofa laini. "Unakunywa nini mgeni wangu?" Akauliza kwa madaha.

"Juisi yoyote ile."

"Leo umekuwa mwanafunzi? Mbona wakati ule kule kwenye disco niliona kama wewe na rafiki yako mlikuwa mkinywa bia?"

"Bia huwa nakunywa kwa sababu maalum tu Edina, siyo muda wote wa kunywa pombe."

"Okay"

Alikwenda kwenye friji na kutoa boksi la juisi, pamoja na mrija, akamletea mgeni wake. Yeye mwenyewe mkononi alikuwa ameshika bia laini mkononi.

Kilipita kimya kama cha dakika mbili hivi, kila mmoja akionekana kutafakari cha kuanzia.

"Enhee lete stori." Edina aliovunja ukimya.

"Mimi hapa ni mgeni, kumbuka wewe ndiye uliyenitafuta, ukaja nyumbani unanichukua, nadhani wewe ndiyo utakuwa una cha kuniambia kwa nini umenileta hapa."

Edina aliguna, mguno uliotaka kuwa kama kicheko hivi.

"Sikutarajia kama Kadili unaongea hivi. Kumbe na wewe muongeaji eee? Kule tulipokuwa tunakutana kwenye disco ulikuwa unaongea kwa kifupi tu, ulionekana mpole sana, lakini leo naona umebadilika, au kule ulikuwa unaficha makucha?" Edina alimtania swahiba yake.

"Hapana, mwenye makucha ana makucha tu, hata kama akiyaficha anajulikana tu kama ana makucha. Mfano paka au simba, hata kama kificha makucha si utajua tu anayo."

Kicheko kilimtoka Edina. "Eee mwenzetu siku hizi umekuwa mwanafalsafa, hongera."

"Ahsante." Alikohoa kidogo na kuuliza.

"Hapa umekuja kwa muda mfupi au?"

"Niko hapa kwa miezi miwili sasa. Nimelipia kwa miezi mitatu kuishi hapa, bado mwezi mmoja pesa niliyolipia iishe."

Kadili hakutaka kujichosha sana kujua alipopata pesa ya kulipia hoteli ya kisasa kama hiyo kuishi kwa miezi mitatu kwa sababu Edina ni mtoto wa kitajiri.

"Si nilisikia umeolewa mumeo yuko wapi?"

"Ulisikia wapi?"

"Kwani siri Edina? Mimi mwenyewe niliona kwenye gazeti umefunga ndoa ya Dk. Deus Kapilima na picha kabisa umepiga na mumeo."

Edina alinyamaza kidogo, akanywa funda kadhaa za bia yake akaiweka kwenye meza.

"Ni hadithi ndefu sana Kadili." Sasa aliongea kwa utulivu na hisia.

"Sijui nianzie wapi?"

"Mimi nakuomba uanzie wakati ule tulipokuwa tunakutana kule disco. Mara ukatuambia kuwa umepigwa marufuku kuja 'blue star'. Baadaye wakaja kunikamata mimi sijui wale jamaa mabausa walipajuaje nyumbani? Nadhani hapo ndipo anzia."

"Kadili unakumbuka wakati ule nilipokuuliza kuwa unaishi wapi ukaniambia Tandale?"

"Ndiyo?"

"Kuna mlinzi mmoja alisikia, ndiyo aliyesema nyumbani kuwa unaishi Tandale, nadhani swali lako nitakuwa nimekujibu." Alisema na kuongeza.

"Kwa ufupi ni kwamba mama yangu mzazi ambaye kwa sasa ni marehemu kwa muda mrefu alikuwa anataka mimi niolewe. Tena niolewe na wanaume ambao anawafahamu yeye na si mimi. Alikuwa listi ya wanaume ambao ni matajiri, wafanyabiashara wakubwa, madaktari bingwa, wanasiasa, na mastaa wengi, lakini mimi nilikataa kwa sababu sikuwa nashirikishwa. Huwezi kuolewa na mtu ambaye humpendi, au umeletewa tu, hamfahamiani."

Baada ya kuona juhudi zake ninashindwa, alitaka kujua sababu ni kwa nini mimi nakataa kuolewa, tena na watu wazito nchini, wenye nyadhifa serikalini, na wafanyabiashara wakubwa.

Badala ya kuona kuwa nalazimishwa kuolewa na mtu nisiyempenda, yeye akawauliza mabaunsa huko anakokwenda kama wanaona kuna mtu ananizuzua." Alinyamaza kidogo na kunywa bia yake.

Alikuwa kama kuna kitu anafikiri akaendelea.

"Mabaunsa waliokuwa wananilinda wakamwambia mama kuwa hawajui na wala hawajamuona mtu yoyote anayeonekana kuwa ana uhusiano na binti yako, ila huwa anapokwenda discho huwa anacheza na kijana mmoja hivi."

"Ndiyo mimi huyo?" Kadili alidakia. "Sasa kumbe nani?" Alijibu huku alijitingisha na kumuangalia jicho la mzaha.

"Mama akawauliza akienda disco huyo binti yangu huwa anacheza na watu tofauti au kila wiki akifika huko anacheza na huyo huyo? Wakajibu huwa anacheza na yeye huyo huyo. Akawauliza hawadhani kuwa huyo ndiye anaweza kuwa anamdanganya binti yake na kumfanya awe anakataa wachumba, wakamjibu hawajui kwa sababu hawana uhakika na hilo.

Baunsa mmoja akamwambia hadhani kuwa yule kijana ni mpenzi wake kwa sababu huwa wanakutana disco tu na kucheza muziki na hawajawahi kumuona wakiwa naye sehemu nyingine yoyote ile, lakini pia wakaona kama vile eti huendani na mimi, wewe ni kijana sana, lakini pia unaonekana umetoka kwenye familia fukara." alizidi kupasua.

Kadili alikuwa ametulia tuli kama maji ya mtungini. Hadithi ile ndiyo alikuwa akiihitaji kuliko kitu kingine chochote.

Siku zote alikuwa akitaka kujua ni kitu gani kilitokea huko nyumbani kwa kina Edina hadi yeye akafuatwa nyumbani na mabaunsa, akatekwa na kutolewa maneno ya kifedhuli na jeuri, pamoja na kuteswa vikali, pia alitaka kujua ndoa ya msichana huyo ilivyofanyika, kwa nini alimtoroka mumewe na sababu ya kifo cha mama yake.

Sababu alikuwa anazisikia kijuujuu, lakini leo kwa sababu yuko ana kwa ana na Edina, basi kila kitu kitakuwa wazi.

"Mama alikaa na kufikiri, hakukubali, akaona huyo anayecheza naye muziki ndiyo atakuwa mpenzi wake.

Siku moja akawaita na kuwauliza kwani huyo kijana anaishi wapi, mmoja akasema alitusikia siku ile tulipokuwa tunafahamiana, ndiyo akamwambia anaishi Tandale kwa Mtogole.

Nilivyopata taarifa baadaye ni kwamba kuna baunsa mmoja alitumwa na mama hadi Tandale na kuja kuchunguza na kuuliza, hadi akapajua. Aliporudi kesho yake alichukua wenzake ndipo alipokuja kukukamata." Edina alimtazama kwa makini Kadili ili kumuona amepokeaje taarifa hiyo.




"Wewe hukuhusika kabisa kuwatajia ninapoishi?"

"Kadili bwana, sasa mimi nimeshawahi kufika kwenu hata siku moja?"

"Basi kwa mawazo yangu mimi nilijua wewe ndiye uliyewaambia, na nikajua labda umelazimishwa."

"Nilazimishwe? Hata wangeniwekea kwenye tanuri la moto, nisingesema."

"Kwa nini?"

"Yaani nikusaliti wewe? Haiwezekani na haitowezekana. Nilikuomba mwenyewe tucheze muziki, ina maana mimi ndiye niliyekuwa na dhima ya kukulinda, ingekuwa ni dhambi kubwa kukuuza."

Kadili aligundua upendo mkubwa ndani ya moyo wa Edina."

"Enhee ikawaje?"

"Nadhani yaliyotokea baada ya hapo wewe unayajua, nisingetaka kuyarudia kwa sababu yanaumiza, ukateswa na kudhalilishwa pale mbele ya kadamnasi ya wafanyakazi wa mama. Kama uliniona mimi nilikaa chini kabisa maana nilichukia na wala sikutaka kuongea kitu chochote."

"Ndiyo, nakumbuka marehemu mama yako, alisema kuwa wewe ulilia sana kunitetea, vinginevyo angeniua."

"Wala hakuongopa. Wanaoingizwa mle ndani kwa sababu za kukiuka maagizo, masharti yake hasa ya kibiashara, ya kibinafsi na sababu kama zako hivyo, huwa hawatoki salama, wanauawa na kuzikwa ndani mle mle. Mama yangu Kadili namjua mwenyewe, alikuwa ni mafia, alijuana na watu wengi wakubwa ambao wanamlinda. Angeweza kufanya chochote na akahonga, asichukuliwe hatua. Nilijua kabisa na wewe yakakukuta, utauawa. Nikalia na kumwambia mama kuwa kijana wa watu asifanyiwe lolote baya, akakataa.

Nikamwambia kama mtamuua Kadili basi na mimi nitachukua kisu na kujiua papo hapo.

Hili lilimtisha mama na siku ya pili akaniambia sitomuua, bali tutampa adhabu kidogo na kumuachia, nikaona heri nusu shari kuliko shari kamili, lakini nikawaambia adhabu mtakazotoa zisimuathiri kiafya, vinginevyo hakuna mtakachokuwa mmefanya ni sawa na kumuua tu."

Kadili alimtazama kwa makini Edina. Alitambua ndani yake kuna kitu zaidi ya upendo. Ni mtu ambaye amemsabishia matatizo bila kukusudia. Lakini akamtetea mbele ya mama yake na watumishi wake ambao nia yao ilikuwa ni kumpoteza duniani.

*Itaendelea Jumamosi*

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

### NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie*

*0767 223 311*

### WACHIMBAJI VISIMA:

Visima Tanzania, tunachimba visima virefu na vifupi kwa gharama nafuu, na ofa ya pampu ya bure simu: 0623528465/ 0658910584.

Pata Ramani za majengo mbalimbali kama Nyumba na Shule

**Simu: 0744113969**

**IN THE REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE COURT OF RESIDENT MAGISTRATE OF MBEYA**
**AT MBEYA**
**COMMERCIAL CASE NO.3 OF 2019**
**NMB BANK PLC....................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**LAUDEN EDWARD MBAMBA.......1ST DEFENDANT**
**SARAH OKIMGI MWITIKA...........2ND DEFENDANT**
**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

TO: 1. LAUDENT EDWARD MBAMBA
2. SARAH OKING MWITIKA

TAKE NOTICE THAT,the plaintiff has instituted a suit against you with the particular claim set out in the plaint filed in this court.Service of summons has been ordered by meaning ofPublication you are hereby summons to to appear in this court in person or by an advocate or by agent dully authorized on 19th day of November,2019 at 08:30 am when this suit will be heard for an Ex-part Judgement.

TAKE FURTHER NOTICE that in default to enter appearance in this court on the day and time mentioned above the suit will proceed and delivered ex-parte judgement may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this 11th day of November, 2019.

115520402

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

JOSEPHAT DHAHABU anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya YAMAHA CRUX yenye namba za usajili MC 396 BCV.Chassis No.* MEIFE4348B2008821* . Engine No. 1DE1008803

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/474333/2019.

115520202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;232/2019
Ombi la MANSUR PAUL ZUBERI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ATHUMANI RASHID

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/11/2019

115519902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI**
**MWANZA**
**MADAI TALAKA 83/2019**
**FROLA ERNEST**
**NJENO.........................................MDAI**
**PASCHAL PETER**
**NGUSA................................MDAIWA**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai alietajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako kuhusiana na madai ya Talaka, Unatakiwa kufika katika Mahakama hii mnamo tarehe 21/11/2019 saa 2:30 asubuhi kujibu madai yaliyotolewa dhidi yako.

KUMBUKA KUWA: Usipohudhuria siku hiyo shauri litasikilizwa na kuwamuliwa bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14/11/2019.

115519702

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 85 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late ANTONY LOLO JEREMIA of Kizota Area within Dodoma Region.**

**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY HELLENA JEREMIA LOLO**

**GENERAL CITATION**

(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 27 Day of November, 2019.

Date at Dododma this 7TH day of October, 2019
...................................................................
PETITIONER

115520002

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# IBRAHIMOVIC

## ATAMANI KUTUNDIKIA DALUGA ITALIA

**LOS ANGELES, Marekan**

ZLATAN Ibrahimovic anataka kumaliza kipindi chake cha kucheza soka nchini Italia, kwa mujibu wa Kocha wa LA Galaxy, Guillermo Barros Schelotto.

Ibrahimovic alibainisha Jumatano wiki hii kwamba hataongeza mkataba wake na miamba hao wa Ligi Kuu ya Marekani (MLS), LA Galaxy, ambako nyota huyo alitua hapo akitokea Manchester United mwaka 2018.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain amekuwa akihusishwa mno na kurudi Ulaya, huku Kamishina wa MLS, Don Garber akibainisha wiki iliyopita kwamba AC Milan ndio inayoongoza kwa kutaka kumsajili kama mchezaji huru.

Napoli, Bologna na Roma nazo ni klabu ambazo zimekuwa zikiwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden, huku pia klabu ya Ligi Kuu ya Australia, Perth Glory nayo ikionyesha nia ya kutaka kumsajili Ibrahimovic.


Alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Ibrahimovic, bosi huyo wa Galaxy, Schelotto aliiambia redo Kiss Kiss: "Hajui nini atakifanya kwa sasa.

"Ni mchezaji wa maajabu, lakini sijui nini kitafuata kwake pengine atamalizia soka lake jijini Naples au Milan.

"Sijui wapi atakwenda, lakini anastahili na anataka kumalizia soka lake nchini Italia."

Ibrahimovic alitumia misimu miwili akiwa na Milan akishinda mataji ya Serie A na Supercoppa Italiana kabla ya kuondoka mwaka 2012 kwenda nchini Ufaransa kwa miamba PSG, ambako alifanya kazi na kocha wa sasa wa Napoli, Carlo Ancelotti.

"Wanajua vizuri," alisema Schelotto.




## GIROUD, GRIEZMANN WAIBEBA UFARANSA IKIFUZU EURO 2020

**PARIS, Ufaransa**

OLIVIER Giroud na Antoine Griezmann walitumia vizuri mazungumzo kipindi cha mapumziko kutoka kwa kocha Didier Deschamps na wakawa nguzo ya ushindi kwa Ufaransa wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Moldova.

Shukrani kwa sare ya bila kufungana kwa Uturuki na Iceland kwenye mchezo uliopigwa mapema wa Kundi H, Ufaransa sasa imefuzu kucheza Euro 2020.

Hata hivyo, makosa ya Clement Lenglet yaliizawadia Moldova bao la kuongoza, huku Raphael Varane akitumia makosa ya Alexei Koselev kuisawazishia Ufaransa.

Kuimarika kwa kipindi cha pili kwa Les Bleus hao, kukamfanya Giroud kufunga bao la ushindi.

Giroud sasa amefunga katika mechi zake zote tatu alizoichezea Ufaransa na mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018 amekuwa na mapenzi makubwa kwa kocha wake.

"Tungefunga mechi kabla ya penalti," alisema Giroud akiiambia Televisheni ya M6.

"Hatukuanza vizuri. Tulikosa umakini mkubwa katika kipindi cha kwanza, lakini tulirudi mchezoni kipindi cha pili."

Naye mshambuliaji wa Barcelona, Griezmann alikazia kwenye kauli ya Giroud, huku pia akishutumu wakicheza vibaya kipindi cha kwanza.

"Ni kweli kwamba, hatukuwa na mchezo mzuri hasa kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili tulirudi mchezoni," alisema Griezmann akiwambia waandishi wa habari.



## MORATA AWATUPIA DONGO WACHEZAJI WA CHELSEA

**MADRID, Hispania**

ALVARO Morata amesema wachezaji wenzake wa timu yake ya zamani ya Chelsea walimfanya aonekane kama vile hajui kucheza mpira.


Raia huyo wa Hispania ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Atletico Madrid, huku kukiwa na uwezekano wa kusajiliwa rasmi kwa pauni milioni 58 mwakani.

Maisha yake pale kwenye dimba la Stamford Bridge yalikuwa yasiyovutia huku wachezaji wenzake wakimfanya ajione hakuwa na uwezo wa kuufanyia mpira jambo lolote zuri ndani ya uwanja.

Morata mwenye umri wa miaka 27, aliambia COPE: "Nina furaha kwa sasa. Hakikuwa kipindi kizuri katika maisha yangu ya soka, sikuwa nafurahia kabisa. Ilifika kipindi hata mimi mwenyewe nilikuwa sijiamini."

Morata alisajiliwa na Chelsea kwa ada ya pauni milioni 65 mwaka 2017 na hakuwa na wakati mzuri na kumfanya aishie kuanzishwa mara 35 tu kwenye mechi za Ligi Kuu England na baadaye kutimkia Atletico katikati ya msimu uliopita.

Alifunga mabao 15 kwa miezi 18 aliyocheza kwenye Ligi Kuu England na hivyo kushindwa kumshawishi Kocha Maurizio Sarri au aliyekuwa mtangulizi wake, Antonio Conte.



Baada ya Chelsea kufungiwa kusajili, huku wengi wakifiri Kocha Frank Lampard angezuia uhamisho huo wa Atletico, lakini aliruhusu na kuamua kubaki na Tammy Abraham, Michy Batshuayi na Olivier Giroud.

Lakini sasa Morata amekuwa kwenye kiwango kikubwa pale Atletico akifunga katika mechi 13 alizochezea kikosi hicho cha Kocha Diego Simeone.

## HABARI MICHEZO

# KUFUZU AFCON 2021

## KENYA YAIBANA MISRI KWAO, COMOROS YATAKATIA TOGO




**CAIRO, Misri**

MISRI ilitoka sare ya kufungana bao 1-1 na wageni Kenya huku Comoros wakiwafunga Togo 1-0 kwenye mchezo wa Kundi G kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika, Afcon, 2021, iliyopigwa juzi.

Kwingineko, Msumbiji iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Rwanda.

Katika mchezo wa Misri na Kenya ambao ulipigwa kwenye dimba la Borg El Arabia jirani na mji wa Alexandria, mabao yote yalifungwa kutokana na makosa ya wachezaji.

Kenya walianza kuizawadia bao Misri ambayo ilikuwa bila Mohamed Salah ambaye ni majeruhi kwa makosa ya Eric Ouma aliyerudisha mpira nyuma kimakosa zikiwa zimesalia dakika tatu kwenda mapumziko na likafungwa na Mahmoud 'Kahraba' Abdel-Moneim ambaye alimfunga kiurahisi golikipa Ian Otieno ambaye baadaye alitolewa.

Kenya ilisawazisha bao hilo dakika ya 67 wakati golikipa wa Misri, Mohamed El Shenawy na mlinzi wake, Ahmed Fathi walipojichanganya na hivyo mpira ukamkuta Michael Olunga (pichani) anayecheza soka la kulipwa nchini Japan na akafunga kwa urahisi.

Kulikuwa na mshituko kwenye mchezo mwingine wa Kundi G mjini Lome wakati kikosi cha Claude Le Roy cha Togo kikichapwa na Comoros nyumbani.

Comoros ilipata bao lake dakika sita baada ya mapumziko likifungwa na Faiz Selemanie anayecheza soka nchini Ubelgiji na kuwafanya kupaa kileleni mwa kundi baada ya mchezo mmoja.

Nayo Msumbiji ilikuwa mshindi kwenye mchezo wa kundi lake la F dhidi ya Rwanda kwenye mchezo uliopigwa jijini Maputo.

Wenyeji walipata bao hilo dakika ya 27 kwa mkwaju wa penalti na likafungwa na Telinho.

**Matokeo yote Afcon:**
**Alhamisi:**
Mali 2-2 Guinea (Kundi A)
Ghana 2-0 Afrika Kusini (Kundi C)
DR Congo 0-0 Gabon (Kundi D)
Msumbiji 2-0 Rwanda (Kundi F)
Misri 1-1 Kenya (Kundi G)
Togo 0-1 Comoros (Kundi G)
Algeria 5-0 Zambia (Kundi H)

**Jumatano:**
Namibia 2-1 Chad (Kundi A)
Malawi 1-0 Sudan Kusini (Kundi B)
Burkina Faso 0-0 Uganda (Kundi B)
Sudan 4-0 Sao Tome and Principe (Kundi C)
Angola 1-3 Gambia (Kundi D)
Jamhuri ya Kati 2-0 Burundi (Kundi E)
Cameroon 0-0 Cape Verde (Kundi F)
Guinea Bissau 3-0 Eswatini (Kundi I)
Senegal 2-0 Congo (Kundi I)
Nigeria 2-1 Benin (Kundi L)
Sierra Leone 1-1 Lesotho (Kundi L)

# Sterling afunguka Gomez kuzomewa



**LONDON, England**

RAHEEM Sterling amewajia juu mashabiki wa timu ya Taifa ya England kwa kumzomea Joe Gomez wakati wa mchezo wa Alhamisi wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Montenegro kwenye michuano ya kufuzu Euro 2020.

Gomez alizomewa wakati alipoingizwa kipindi cha pili kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Wembley, ambapo ushindi huo wa England uliwafanya wakate tiketi ya kufuzu kwa michuano hiyo mwakani. Beki huyo wa Liverpool alikwaruzana na Sterling wakati wa mchezo wa Ligi Kuu England Jumapili iliyopita baina ya timu hizo na nyota huyo wa Manchester City alitemwa kwenye kikosi cha England baada ya tukio hilo.

Sterling hakufurahishwa na mashabiki wa England ambao walimzomea Gomez, akisema kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, hakuna kibaya alichokifanya.

"Kwa mashabiki wote wa England, nilitaka kuacha mambo yaende kama yalivyo, lakini natakiwa kuzungumza tena," aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Ulikuwa wakati mgumu kwangu kuona mchezaji mwenzangu akizomewa kwa tukio hilo ambalo mimi ndio nilikuwa mhusika.

"Joe hakufanya jambo lolote baya na kwangu mimi kuona akizomewa, hilo si sawa, kwani hawakumtendea haki."

Katika ushindi huo wa England, mabao yake yalifungwa na Harry Kane aliyefunga 'hat-trick', Alex Oxlade-Chamberlain, Marcus Rashford, Tammy Abraham na Aleksandar Sofranac aliyejifunga.

## Ramos atamani kuitwa kukipiga Olimpiki 2020

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos ameonyesha nia yake ya kutaka kuiwakilisha Hispania kwenye michezo ya Olimpiki mwaka 2020.

Ramos ambaye ni beki na nahodha wa Klabu ya Real Madrid na nchi yake, ndiye mchezaji aliyeichezea mechi nyingi zaidi Hispania akicheza 168.

Hajawahi kushiriki kwenye michezo ya Olimpiki, hata hivyo kwenye mchezo wa soka katika mashindano hayo yanayoruhusu wachezaji chini ya umri wa miaka 23, inaruhusiwa kuchagua wachezaji watatu waliozidi umri huo.

Ramos ambaye ni mlinzi wa kati wa muda mrefu wa Hispania akiwa na upatina na Gerard Pique, amepaza sauti yake kutaka kushiriki kwenye michezo hiyo itakayofanyika jijini Tokyo nchini Japan mwaka 2020.


"Inanipa hamasa kubwa wakati wote ninapoiwakilisha Hispania. Kama Pique, wachezaji wote ambao wanaweza kucheza michezo ya Olimpiki pamoja na Hispania watafanya hivyo," alisema Ramos akiwaambia waandishi wa habari wakati wakijiandaa kuelekea mchezo wao wa kufuzu Euro 2020 dhidi ya Malta.

"Kwanza kuna Euro na halafu tutaangalia, lakini nimehamasika mno kwa sababu ni kitu ambacho sijawahi kupata uzoefu wake."

Ramos atafikisha umri wa miaka 34 Machi mwakani, lakini hana mpango wa kutundika daluga zake.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ASAKA MAWILI KUFIKISHA 100 KIMATAIFA

Atupia hat-trick tisa timu ya taifa wakati wakibakiza ushindi mmoja kufuzu Euro 2022, huku...

**Lisbon, Ureno**

CRISTIANO Ronaldo atakuwa na nafasi ya kufikisha mabao 100 timu ya taifa wakati Ureno itakaposafiri kwenda kuivaa Luxembourg Jumapili.

Ronaldo juzi alifikisha mabao 98 kimataifa kufuatia kutupia hat-trick dhidi ya Lithuania na kuifanya Ureno kuhitaji ushindi mmoja kuweza kufuzu Euro 2020.

Mshambuliaji huyo wa Juventus mwenye umri wa miaka 34, Ronaldo, anaweza kuwa mtu wa pili duniani kufikisha mabao 100 kimataifa kama Jumapili atafunga mara mbili dhidi ya Luxembourg.

Aidha, Ronaldo sasa amefikisha hat-trick tisa timu ya Taifa ya Ureno na saba kati ya hizo zilipatikana tangu aliposheherekea kufikisha miaka 30 hivyo sasa amebakisha mabao 11 kumfikia nguli wa zamani wa Iran, Ali Daei, anayeshikilia rekodi ya dunia ya mchezaji mwenye mabao mengi zaidi (mabao 109) kwa timu ya taifa.

Nahodha huyo wa Ureno alifunga bao la mapema kwa mkwaju wa penalti kabla ya kuongeza la pili dakika ya 22.

Afonso Fernandes (dakika ya 52), Mendes Paciencia (dakika ya 56), na kiungo wa Manchester City, Bernardo Silva (dakika ya 63) wote walifunga kabla ya Ronaldo kurudi tena kambani kukamilisha hat-trick yake dakika ya 65.

Ronaldo alifanyiwa mabadiliko ('sub') katika mechi mbili zilizopita za Juventus, na kocha wa timu hiyo, Maurizio Sarri akasema alikuwa majeruhi wa goti.

Lakini Kocha wa Ureno, Fernando Santos amesema: "Kamwe sikuwa na shaka yoyote kuhusu hali yake, walikuwa ni watu wengine waliokuwa nayo. Hakuna kinachonishangaza kuhusu Cristiano."

Mabingwa watetezi, Ureno watafuzu kwa fainali zijazo za Ulaya kama wataifunga Luxembourg Jumapili.

Aleksandar Mitrovic alifunga mara mbili wakati Serbia ikiifunga Luxembourg mabao 3-2 kujihakikishia mbio hizo za kufuzu kwa kushika nafasi ya pili, hivyo hatima ya Kundi B sasa kusubiri mechi za mwisho. Ukraine tayari imeshatinga Euro 2020 kama kinara wa kundi hilo kutokana na kufikisha poiti 19 ambazo haziwezi kufikiwa na Ureno yenye alama 14 wala Serbia yenye pointi 13 ikiwa katika nafasi ya tatu.

## KWA UFUPI

**DORTMUND NAYO KWA GIROUD**
BORUSSIA Dortmund imejiunga na Inter Milan katika mbio za kutaka kumsainisha mkataba mshambuliaji asiyepewa nafasi Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, 33. ***(Mirror)***

**HAALAND KUMFUATA SOLSKJAER**
MANCHESTER United inapewa nafasi zaidi katika mbio za kuinasa saini ya mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Mnorway Erling Braut Haaland, 19, ambaye alinolewa na Ole Gunnar Solskjaer wakati akiinoa Molde. ***(Dagbladet - in Norwegian)***

**COUTINHO AMTESA POCHETTINO**
SUALA moja linalomtesa Kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino klabuni hapo ni kitendo cha kushindwa kumsajili kiungo Mbrazil Philippe Coutinho kutoka Barcelona majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alihitimisha kwa kujiunga na Bayern Munich kwa mkopo. ***(Sun)***

**LIVER, NAPOLI KWA BERGE**
LIVERPOOL na Napoli ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kiungo wa Genk, Mnorway Sander Berge, 21, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Dimitri de Conde. ***(Radio Punto Nuovo, via Goal)***

**MANDZUKIC KUWAHI UNITED**
MANCHESTER United inatumai kufikia makubaliano na mshambuliaji wa Juventus, Mcroatia Mario Mandzukic, 33, kuanza kujifua na klabu hiyo mwezi ujao kabla ya dirisha la usajili la Januari. ***(Tuttosport - in Italian)***

**XHAKA AIVUTIA NEWCASTLE**
NEWCASTLE United inavutiwa kumsajili kiungo wa Arsenal, Mswisi Granit Xhaka, 27, kwa mkopo wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Telegraph)***

**ATLETICO KUMFUATA RAKITIC**
ATLETICO Madrid ipo tayari katika usajili wa dirisha dogo la Januari kumfuata kiungo wa Barcelona na Croatia, Ivan Rakitic, 31, ikiwa na pauni milioni 35. ***(Movistar, via Mail)***

**MILAN KWA IBRAHIMOVIC**
AC Milan ipo tayari kumsajili mshambuliaji Msweden Zlatan Ibrahimovic, 38, katika dirisha la Januari wakati huu akiwa mchezaji huru, lakini mpango huo unahitaji idhini ya Mkurugenzi Mkuu, Ivan Gazidis. ***(Calciomercato)***

**BECKHAM AMPANIA MODRIC**
DAVID Beckham anatumai kumfanya kiungo wa Real Madrid, Mcroatia Luka Modric, 34, kuwa nyota wake mkubwa kusajiliwa katika klabu yake mpya ya Inter Miami. ***(AS)***

**BELLERIN AMULIKWA ITALIA**
WAKALA wa beki wa Arsenal, Mhispania Hector Bellerin, 24, amesema mteja wake "anaona namna msimu unavyokwenda" hapo Emirates baada ya kupokea ofa kutoka Italia. ***(Sky Sport Italia via Football Italia)***

**EMRE CAN AWINDWA UNITED**
JUVENTUS inaweza kumtoa kiungo Mjerumani Emre Can, 25, taarifa za kuwindwa na Manchester United, kwamba anapatikana kwa ada pungufu ya dirisha la Januari. ***(Calciomercato - in Italian)***



# KILIMANJARO QUEENS MORALI JUU IKIIVAA SUDAN CHAMAZI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Queens, inashuka dimbani leo dhidi ya Sudan Kusini katika mechi ya ufunguzi ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge) kwa Wanawake, ikiwa na lengo moja tu la kulibakisha kombe hilo nchini, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Bakari Shime.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema kikosi hicho kipo vizuri kwa ajili ya mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Chamazi na kueleza amewapa mazoezi ya kutosha.

"Maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yanaendelea vizuri, wachezaji wote wapo vizuri kila mmoja ana morali ya ushindi," alisema.

Alisema kila mchezaji ameahidi kujituma kuhakikisha kombe hilo linabaki nyumbani, ukizingatia wao ndio wenyeji wa mashindano hayo.

Kocha huyo alisema anaziheshimu timu zote ambazo zinashiriki mashindano hayo kwa kuwa zina viwango vizuri.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kuisapoti timu hiyo inapokuwa dimbani ili icheze kwa kujiamini.

Hii ni mara ya tatu, michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kufanyika katika Ukanda huu, ambapo mara ya kwanza ilifanyika 2016 katika mji wa Jinja Uganda na mwaka jana yalifanyika Kigali Rwanda huku Kilimanjaro Queens ikitwaa ubingwa katika kila msimu.

Mwaka huu mashindano hayo yanashirikisha jumla ya nchi nane ambazo ni wenyeji Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), Tanzania visiwani (Zanzibar Queens), Sudan Kusini, Burundi, Uganda, Kenya, Ethiopia pamoja na Djibouti.

NADAKA...



Kipa anayelelewa katika Kituo cha Kufundisha Makipa cha Tanzania Goalkeeping (TGTC), Martin Kaeza, akidaka mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Z'bar Queens yapewa siri ushindi Cecafa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Mohmed Ali Hilali, ameitaka timu ya Taifa ya Wanawake ya Zanzibar (Zanzibar Queens) kuzingatia nizamu katika michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge) kwa Wanawake inayotarajiwa kuanza kesho katika Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam.

Katibu huyo ameyasema hayo hapo jana wakati akiiaga na kuikabidhi bendera ya Taifa timu hiyo wakati ikielekea Tanzania Bara katika michuano hiyo Cecafa ambapo Zanzibar Queens itafungua dimba leo dhidi Burundi.

Alisema ni vema kuzingatia nidhamu katika michuano hiyo ambayo huenda ikawa siri ya mafanikio ya ushindi wao katika michauno hiyo inayoshirikisha nchi nane ambazo ni Zanzibar, Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Burundi, Sudan Kusini, Ethiopia na Djibout.

Alisema anaamini kama wakiwa na nidhamu na kushirikiana kwa pamoja ndani na nje ya uwanja itakuwa ni moja ya sababu ya kupata ushindi mkubwa.

Aidha, Katibu huyo wa ZFF, amewataka Wazanzibar waliopo jijini Dar es Salaam na wale waliopo visiwani Zanzibar kuungana kuishangilia timu hiyo pindi ishukapo dimbani ili kuipa hamasa ya kufanya vizuri.

# Namungo, Ndanda FC kutifuana kirafiki

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kujiweka fiti kabla ya Ligi Kuu kuendelea baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, timu ya Ndanda FC inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Namungo FC Jumapili wiki hii.

Akizungumza na Nipashe jana, msemaji wa timu hiyo, Idrisa Bandali, alisema kikosi chao kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mtanange huo utakaopigwa Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

"Kikosi kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Namungo FC katika mchezo wetu wa kirafiki Jumapili," alisema Idrisa.

Alisema Ligi Kuu msimu huu ina ushindani mkubwa kutokana na kila timu kujipanga vizuri.

Kuhusu usajili wa dirisha dogo ambalo litafunguliwa Desemba 16, mwaka huu, alisema watasajili kipa, kiungo pamoja na kuimarisha safu ya ushambuliaji.

"Nafasi hizo ndio ambazo tunatarajia kuziboresha ili timu yetu iendelee kubaki Ligi Kuu," alisema.

# Cheche: Azam hakuna kulala

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Azam FC umesema kikosi chao kinaendelea na mazoezi ya nguvu katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu imesimama kupisha kalenda ya Fifa ambapo timu mbalimbali za taifa ikiwamo Taifa Stars zinakabiliwa na mechi za kimataifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Idd Cheche, alisema mpaka sasa wachezaji wote wapo vizuri na anaamini watarejea Ligi Kuu wakiwa wameimarika zaidi.

**"Tukipata mchezo wa kirafiki tutawafahamisha, lakini kikubwa kwa sasa tunaendelea na mazoezi ya nguvu ili tuweze kubaki kwenye Ligi Kuu,"alisema kocha huyo huku akiwataka mashabiki kuendelea kuisapoti timu hiyo.**

Azam inashikilia nafasi ya 11 katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 13 baada ya kushuka dimbani mara saba.

Michezo
Jumamosi Novemba 16, 2019
Nipashe



Ronaldo asaka mawili kufikisha 100 kimataifa HABARI UK 30



Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta na mshambuliaji wa timu hiyo, Simon Msuva.

# SAMATTA AWASHANGAA WENZAKE TAIFA STARS

●●● Awataka kumfuata Ulaya ili kuisaidia nchi kimataifa, msuli sasa waelekezwa kwa Libya, Kenya waishika Misri...

**Na Mwandishi Wetu**

ACHANA na matokeo ya Taifa Stars jana dhidi ya Equatorial Guinea kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021, na moja kwa moja geukia kauli ya nahodha wa timu hiyo ya Taifa ya Tanzania, Mbwana Samatta ya kuwataka wachezaji wenzake kufanya uamuzi sasa wa kwenda kucheza soka la kulipwa, utaipenda.

Jana Samatta aliiongoza Taifa Stars katika Uwanja wa Taifa kuivaa Equatorial Guinea, wakati kwa sasa akili yake na wachezaji wenzake wakiielekeza katika kibarua kama hicho Jumanne watakaposhuka dimbani nchini Libya kuwavaa wenyeji wao hao katika mechi ya pili ya Kundi J.

Hata hivyo, akiweka kando mechi hizo kilio chake ni kuwaona wachezaji wengi wakigeukia kucheza soka la kulipwa nje ya nchi ili kuisaidia timu hiyo ya Taifa.

Akizungumza na mwandishi wetu siku moja kabla ya kuivaa Equatorial Guinea, alisema anashangazwa na wachezaji wengi wa Tanzania kufurahia zaidi kuendelea kucheza soka nchini, licha ya juhudi ambazo amekuwa akizionyesha katika kuwatafutia timu nje ya nchi.

Alisema wachezaji wengi wamekuwa wakihofia kwenda kucheza soka nje na ameshindwa kujua wanachokihofia jambo ambalo amekuwa akiwaza pengine hofu yao ni kwa maneno ya watu endapo watashindwa.

"Tunapita njia tofauti, sijui wao wanapita wapi, naona wachezaji wetu wapo 'comfortable' kucheza hapa nyumbani, kuna watu wengi nazungumza nao kuhusu kuwatafutia timu ila utayari wa wachezaji, sijui wanaogopa nini.

"Nilifurahi wakati nakuja kujiunga na Taifa Stars nilikutana na Msuva (Simon) Ulaya, tukaja pamoja, natamani siku moja tukutane hata nane tukija kujiunga na timu ya taifa," alisema Samatta ambaye alionyesha kiwango cha juu kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool wakati akiifungia timu yake ya KRC Genk wakilala kwa mabao 2-1 katika Uwanja wa Anfield wiki iliyopita.

**Kenya yaidindia Misri**

Ukiachana na matokeo ya jana, juzi Kenya iliinga'ngania Misri nyumbani kwa kuilazimisha sare ya bao 1-1 katika mechi ya Kundi G ya kuwania kufuzu Afcon 2021.

Huku mchezo mwingine wa kundi hilo Comoros ikishuhudiwa ikifanya maajabu ugenini kwa kuibanjua Togo bao 1-0 na kukaa kileleni mwa Kundi G.

# Kagere ashindwa kutoboa Msumbiji

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI hatari wa Simba, Meddie Kagere, ameshindwa kufurukuta mbele ya safu ya ulinzi ya Msumbiji baada ya kushindwa kuisaidia timu yake ya Taifa ya Rwanda wakati ikichezea kichapo cha mabao 2-0 ugenini juzi.

Kagere na wenzake sasa watalazimika kucheza kufa kupona Jumanne katika mechi ya pili ya Kundi F kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021, wakati watakapowakaribisha waandaji hao wa fainali hizo.

**Cameroon ambayo tayari ina tiketi ya kushiriki fainali hizo kutokana na kuwa mwenyeji, itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare tasa nyumbani dhidi ya Cape Verde juzi.**

Hata hivyo, Kagere ambaye anaongoza kwa kucheka na nyavu Ligi Kuu Bara, itabidi kufanya kazi ya ziada ili kuibeba Rwanda kutokana na safu ya ulinzi ya Cameroon kuwa imara na ikiundwa na wachezaji wazuri wanaocheza soka la kulipwa.

Hadi sasa wakati Simba ikiwa kileleni mwa Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara tisa msimu huu, Kagere amecheka na nyavu mara nane na kuiwezesha kuvuna pointi 22.

Na katika orodha ya wafungaji vinara, Kagere yupo kileleni akifuatiwa na Paul Nonga na Daruesh Saliboko wanaoichezea Lipuli FC, ambao kila mmoja ana mabao sita wakati huu timu yao ikishika nafasi ya tano ikiwa na alama 15 baada ya kushuka dimbani mara tisa kama Simba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >